# Nipashe

Jumatano Agosti 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581047

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,025,118,259

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Kampuni** yadaiwa kutapeli wakulima Sh. bilioni saba

UKURASA 3



TEN HAG FURAHA TUPU KUITUNGUA LIVERPOOL

UKURASA 21



# Zaidi ya kaya 7,000 zahesabiwa

• **Mmoja** afariki baada ya kusensabika, karani aporwa kishikwambi, mwingine aenda nacho kilabuni... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MIAKA MITANO JELA KUJIFANYA MKURUGENZI USALAMA WA TAIFA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Iyonga Mlele, mkoani Katavi, imemuhukumu...

## Kikwete aeleza alivyofanya kazi pamoja na Mrema



UKURASA 3



Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongela (wa pili kushoto), akigawa nyamapori kwa wananchi jamii ya Wahadzabe ili kuwahamasisha wahesabiwe katika Kitongoji cha Murus Mang'ola, Kijiji cha Kangded, wilayani Karatu jana. **Picha ndogo:** Karani wa Sensa ya Watu na Makazi (aliyekaa chini), akiwahoji wananchi hao baada ya kukubali kuhesabiwa. **Picha zaidi Uk. 18. PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Samia ahesabiwa, awatoa hofu Watanzania maswali ya dodoso

UKURASA 2

**MICHEZO** **MANZOKI ATUA RASMI DAR** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na karani wa Sensa ya Watu na Makazi, Phausta Ntigiti, wakati alipokuwa akihesabiwa katika makazi yake Chamwino, Ikulu mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Zaidi ya kaya 7,000 zahesabiwa

**Na Waandishi Wetu**

KAYA 7,768 zimehesabiwa mpaka majira ya saa tano asubuhi jana ikiwa ni utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika kwa siku saba.

Matukio mbalimbali yalijitokeza likiwamo la mtu mmoja kufariki dunia baada ya kuhesabiwa, karani kuporwa kishkwambi, mwingine akienda na kifaa cha sensa kilabuni na wengine wawili wakisimamishwa kazi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema kazi ya kuhesabu watu iliendelea vizuri jana na mwitikio ni mkubwa.

Takwimu hizo zilikusanywa na makarani katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo waliolala kwenye nyumba za wageni na wasafiri.

Dk. Chuwa alitoa taarifa hiyo jana baada ya kukagua kituo cha upokeaji taarifa za sensa ya watu na makazi (Data center), kilichoko Njedengwa jengo la Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Akihutubia taifa kupitia vyombo vya habari juzi, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema matokeo ya awali ya sensa hiyo yatatolewa Oktoba, mwaka huu.

Alisema sensa hiyo ina umuhimu wa kipekee kwa vile imeunganishwa na sensa ya majengo yote nchini kwa ajili ya kufahamu kiwango cha ubora wa makazi ya wananchi wanayoishi, jambo ambalo halijawahi kufanyika.

**KARANI APORWA KISHIKWAMBI**

Mratibu wa Sensa Jiji la Arusha, Maneno Maziku, amesema sensa inaendelea vizuri licha ya mmoja wa makarani kuporwa kishikwambi usiku wa jana, wakati wa akienda kuhesabu makundi maalum huku mume wake akijeruhiwa kichwani.

Akizungumza Nipashe jana kwa njia ya simu, Maneno alisema baada ya tukio hilo karani huyo, Sarapia Kiwango, alipewa kishikwambi kingine na kuendelea na kazi.

Diwani wa Kata ya Unga Limited, Mahamod Said na Mtendaji wa Kata hiyo, Sophia Laizer, walisema usiku wa kuamkia jana wakati karani huyo anakwenda kuhesabu makundi maalum, alivamiwa na watu waliokuwa na bodaboda na kumpora kishikwambi hicho.

"Jana usiku hawa makarani wa sensa waliitwa kwa mtendaji, wakati wanakwenda huko ndiyo wakakutana na vibaka waliokuwa kwenye bodaboda wakamjeruhi mumewe na kumpora kishikwambi kisha kutoweka," alisema Mahamod.

Mraribu wa Sensa Mkoa wa Arusha, Leocadia Athanas, alisema inaendelea vizuri licha ya changamoto ndogo.

**WAHADZABE WAPEWA NYAMA**

Mratibu wa Sensa Wilaya ya Karatu, Rose Mipango, alisema zoezi hilo linaendelea vizuri na walianza na makundi maalum, wakiwamo wageni waliolala hotelini, watoto wanaoishi mazingira hatarishi, madereva wa malori pamoja na watalii.

Aidha, alisema Wahadzabe wa Kata ya Baray wilayani Karatu, walichinjiwa nyumbu wawili na pundamilia wawili, pamoja na ndizi mbivu ili wawe nyumbani kuhesabiwa.

Akizungumza baada ya kuhesabiwa, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba alisema, nchi nyingi zinatamani kufanya sensa lakini hazijafanikiwa na kueleza kuwa ni fahari kwa Tanzania kukamilisha na mwitikio ni mkubwa.

Aliwataka makarani kuongeza kasi ya uandishi kuikamilisha kwa wakati ili taifa lipate takwimu sahihi za watu kwa ajili ya maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandiliwa, alisema sensa ndiyo msingi wa maendeleo ya taifa lolote kwa kuwa huwezi kupanga mipango ikaendana na uhalisi kama hujui idadi wa wakazi.

Naye Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Tanga (CCM), Ummy Mwalimu, alitoa rai kwa wananchi wa Tanga kushiriki kikamilifu katika eneo walilolala.

**AFARIKI BAADA YA KUHESABIWA**

Mkazi wa Majengo, Manispaa ya Kahama Mary Maya (40), amefariki dunia saa chache baada ya kuhesabiwa na makarani wa sensa usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Msimamizi wa zamu wa hospitali hiyo, Dorah Ndovi, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho. Pia alisema mgonjwa mmoja alikataa kuhesabiwa akitaka kwanza awaone viongozi wa eneo lake, lakini baada ya kupewa elimu alitoa taarifa.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema katika baadhi ya nyumba za kulala wageni kuna wananchi walikuwa wanataka kugomea kuhesabiwa, lakini baada ya kuelimishwa walikubali.

Diwani wa Kata ya Nyankende Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, Doa Limbu alisema alikuwa wa kwanza kuhesabiwa na mwitikio wa wananchi ni mkubwa na kwamba kuna abiria aliyelala kwenye basi alikataa kuhesabiwa lakini baada ya kuelimishwa alikubali.

Mkazi wa Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala, Ponda Masele, alisema alipigiwa simu na makarani wa sensa na kutoa taarifa zake kwa simu baada ya kufika nyumbani kwake na mke wake kushindwa kujieleza.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mlalakuwa, Kata ya Makongo, Wilaya ya Kinondoni, Rehema Komba, alisema wamepata ushirikiano kwa wananchi na walianza kazi saa sita usiku kwenye makanisa, nyumba za kulala wageni na makazi maalum.

Mkazi wa Ibinzamata mkoani Shinyanga, Albert Silwimba, alisema tangu jana asubuhi alikuwa nyumbani akiwasubiri makarani na ilipofika saa 5:00 asubuhi aliamua kuondoka.

Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mkoa wa Shinyanga, Eliudi Kamendu, alisema kazi hiyo iliendа vizuri jana.

Mkazi wa Kata ya Miembeni mkoani Kagera, Respicius Bwanashamba, alisema sensa ni muhimu kwa maisha ya mtu binafsi na taifa na kwamba sio la mara kwa mara kwa kuwa hufanyika kila baada ya miaka 10.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, baadhi ya wakazi wa Kata ya Nyahanga walisema uchache wa makarani wa sensa ulisababisha wananchi kushindwa kuhesabiwa kwa wakati.

Shija Kashindye alisema ili kazi hiyo ifanikiwe kwa wakati ingetakiwa maswali yakabaki yenye umuhimu.

Grace Festo, mkazi wa Mirongo alisema wamehamasika baada ya kupata matangazo kutoka sehemu mbalimbali hivyo wamelipokea vizuri zoezi hilo.

Naye Omary Kassim, alisema majira ya saa 2:30 asubuhi karani alifika eneo lake na kuhesabu familia yake.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, akizungumzia kazi hiyo alisema kwa siku ya jana ilifanyika vizuri na mpaka mchana walikuwa hawajapokea tatizo lolote.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, amewaonya watakaokwamisha sensa ikiwamo kuiba vishikwambi kuwa ni kosa la jinai, huku akiwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa makarani.

"Makarani watakaotoa siri za sensa tutawakamata mara moja pamoja na yoyote atakayethubutu kuvizia na kuiba visikwambi vya ukusanyaji wa taarifa atakuwa ametutia kwenye hasara na mtu huyo atashughulikiwa kisheria na hatasahau," alionya Mwasa.

***Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA), Oscar Assenga (TANGA), Neema Sawaka na Shabani Njia (KAHAMA), Rose Jacob na Neema Emmanuel (Mwanza), Marco Maduhu, Shinyanga, Restuta Damian (KAGERA),Alphonce Kabilondo (GEITA), Ashton Balaigwa, (MOROGORO), Joram Gervas, Owen Bariki, Isiyaka Nyamihasi, Sabina Ntobi, Camila Bonanza, Saumu Hassan, Aisha Kondo (TUDARCo).**

## Samia ahesabiwa, awatoa hofu Watanzania maswali ya dodoso

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameongoza Watanzania kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi na kuwatoa hofu kuwa maswali yanayoulizwa kwenye dodoso hayana ugumu.

Vilevile, amewashauri kuandaa mapema majibu ya maswali husika ili kuwarahisishia kazi makarani.

Rais Samia alihesabiwa jana na Karani Phauster Ntigiti kwa takribani dakika 30 kwenye makazi yake Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma.

Akizungumza jana baada ya kuhesabiwa, Rais Samia alisema maswali yanayoulizwa ni mengi, lakini yanayojibika.

"Nataka niwatoe hofu wananchi ni kweli maswali ni mengi kidogo, lakini hakuna swali gumu, maswali yote yanajibika kama ni mkuu wa kaya unaijua nyumba yako vizuri maswali yote yanajibika.

"Ombi langu kwa wananchi ni kuweka taarifa zao mapema, kama watu wetu wa takwimu mtu wa takwimu na kamisaa na timu zao walitoa maswali mapema kwa hiyo ni vyema wale ambao hawajapata maswali wayatafute ili waanze kuyatafutia majibu mapema," alisema.

Alitoa mfano vitu vinavyohitajika majibu yake ni kuhusu bima ya afya, aina ya bima mtu anayotumia, namba ya NIDA na kwa wale waliopo Zanzibar inahitajika namba ya kitambulisho cha Mzanzibar.

"Taarifa ukikaa nazo mkononi wanakwenda haraka haraka, sasa kaya zetu tunazijua sio chini ya watu watano hizo ndiyo wastani wa kaya zetu, sasa kupata taarifa za watu watano wakubwa zote kwa ukamilifu kama hamkuwa tayari inaweza kuchukua muda mkubwa," alisema.

Aliwataka makarani kufanya kazi kwa ufanisi na wananchi watoe majawabu yanayotakiwa.

Kwa upande wake, Kamisaa wa Sensa na Spika mstaafu, Anne Makinda alisema: "Alichosema Mheshimiwa Rais hapa kuna wakati unaulizwa namba ya NIDA, leseni ya udereva, nyaraka kama hizi ukiwa nazo sasa hivi vikakaa hapo karibu wakikuita basi unavichukua tu si unajua tena nyumba zetu zilivyojaa wakiita hapo unaenda kutafuta uanze kuchakura huko ndani mpaka vionekane jasho linakutoka na muda unakuwa unaisha."

Alisema sensa hiyo itafanyika kwa siku saba na kuomba wananchi wawe wavumilivu.

"Hawa makarani leo hii wakifanikiwa kwa asilimia 15 tu wakifanikiwa hivyo tunawaomba wananchi wasituchoke sisi maofisa kwamba leo hawakuja makarani...ni siku saba tunaomba utulivu na uvumilivu uwapo, tungekuwa nchi iliyoendelea kila mtu angejisensa mwenyewe kwa kutumia simu yake," alisema.

Aidha, alisema sio kila nyumba itafikiwa siku ya sensa na kutaka waendelee kusubiri kwa muda huo uliotangazwa.

"Kama kaya watakuwa na fomu unaweza ukajaza mule ndani kama una kazi yako unakwenda kazini kwako taarifa ipo nyumbani, karani akifika pale anaweza akatumia ile, lakini akikuta hajapata uelewa vizuri atatumia simu uliyomwekea atakupigia," alisema.

"Tusingependa watu wakae nyumbani wanasubiri eti karani sio hivyo, sio lengo letu, hii ya leo ilikuwa tupumzike wote tuiheshimu siku ya leo lakini tujipange mtu kazi yake anakwenda kuifanya."

Alisisitiza viambatanisho vinavyohitajika kwenye sensa visichakachuliwe kwa kuwa maswali yanayoulizwa sio magumu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu Tanzania (NBS), Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema dodoso lina maswali 100 na sensa hiyo ni ya sita ambayo inafanyika kidigitali.

**DODOMA WALIVYOZINDUA**

Jana usiku, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alizindua sensa wilayani Mpwapwa akiwahimiza wananchi kuhesabiwa.

Uzinduzi huo ulikuwa na shamrashamra hizo ziliambatana na kulipua fataki na kukata keki huku makarani hao wa sensa wakiwa wameshikilia vishkwambi na wamevaa vikoti mng'ao (feflector) tayari kwa kuanza kazi.

Kadhalika, shamrashamra hizo zilifanyika katika Jiji la Dodoma viwanja vya Nyerere (Nyerere Square) na makarani kuanza kazi yao usiku huo kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo hospitali na kumbi za starehe.

Nipashe ilizunguka maeneo ya Jiji hilo ulikuwa tulivu huku baadhi ya maduka yakiwa yamefungwa hasa kwa nyakati za asubuhi.

# Kikwete aeleza alivyofanya kazi na Mrema

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, jana aliungana na viongozi wengine kutoa pole kwa familia ya mwanasiasa mkongwe nchini, Augustino Mrema, huku akielezea alivyomfahamu na kufanya kazi naye.

Kikwete alifika nyumbani kwa Mrema ambaye mpaka anafariki dunia alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Salasala, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Mrema, ambaye aliwahi kuwa kiongozi katika nyadhifa mbalimbali serikalini, ikiwamo Naibu Waziri Mkuu, alifariki dunia usiku wa kuamkia Jumapili iliyopita katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, alikokuwa amelazwa kwa matibabu.

Mwanasiasa huyo anatarajia kuagwa kesho katika ibada itakayofanyika Kanisa la Mtakatifu Augustino, Parokia ya Salasala na kusafirishwa kwenda nyumbani kwao, Kiraracha, Moshi mkoani Kilimanjaro kwa maziko yatakayofanyika kesho.

Akitoa salamu za pole, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alieleza alivyofahamiana na kufanya kazi na Mrema. Alisema alimfahamu Mrema miaka mingi wakiwa makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kisha kufanya naye kazi katika Baraza la Mawaziri.

Mrema alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri Mkuu kabla ya kuwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana wakati Kikwete akiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini na baadaye Waziri wa Fedha katika serikali ya awamu ya pili chini ya Rais (mstaafu) Alhaj Ali Hassan Mwnyi mwaka 1990 hadi 1995.

"Tumefanya naye kazi kwa pamoja kwa karibu. Mwaka 1995 mwenzetu akaenda upande mwingine, sisi tukabaki njia kuu. Pamoja na hayo, Mrema amekuwa rafiki yangu, alikuwa mtu ambaye tumekuwa tukiwasiliana," alisema Kikwete.

Mke wa Mrema, Doreen Mrema, alimshukuru Mungu kwa maisha ya mume wake huku akiwaomba Watanzania kuendelea kumwombe katika kipindi hiki anachopitia.

Pia Doreen aliwashukuru Watanzania wote waliokuwa wakimwombea mume wake kipindi anaugua huku akiishukuru serikali kwa kuendelea kuungana na familia katika kipindi hiki.

Miongoni mwa waliofika jana kutoa pole kwa familia ya Mrema jana ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia na mbunge wa zamani wa Moshi Vijijini, Antony Komu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mbatia alisema kazi ambazo Mrema alizifanya akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi zimeacha alama na hazitafutika na kwamba msimamo na uthubutu wake unapaswa kuigwa na wale wanaoingia kwenye siasa.

Komu kwa upande wake, alisema Mrema wakati anagombea urais mwaka 1995 alikuwa katibu wake wa kampeni na kwamba ni miongoni mwa viongozi ambao walikuwa wanyenyekevu na waliokubali kushuka kusikiliza wananchi bila kujali hali zao.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mama Mariam Mwinyi, wakimsikiliza karani wa Sensa ya Watu na Makazi, Asia Hassan Mussa, wakati wakihesabiwa katika makazi yao, Migombani Ikulu Ndogo jana. **PICHA: IKULU**

# Kampuni yadaiwa kutapeli wakulima bil. 7/-

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na vyombo vingine vya dola kuifanyia uchunguzi Kampuni ya Kilimo ya JATU inayodaiwa kuchukua fedha za wananchi zaidi ya Shilingi bilioni saba ikidai kuwalimia na kunenepesha mifugo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Bashe, wakulima zaidi ya 1,000 waliwasilisha malalamiko yao kwenye wizara yake kwa njia mbalimbali, lakini walipofanya uchunguzi walibaini hukuna mazao mashambani, wala maghala na mifugo inayonenepeshwa kama walivyoahidiwa.

Akizungumza na baadhi ya wakulima hao kwa njia ya mtandao, alisema baada ya kupokea malalamiko yao yaliyowasilishwa kwake kwa njia ya mitandao ya kijamii, alituma timu ya wataalamu kufanya uchunguzi kwa wiki moja na kubaini udanganyifu huo.

"Niliwaahidi nitawasilikiza na nitafanya kazi, nilichokifanya leo niwaite na menejimenti ya JATU iwepo ni kuangalia fedha walizokusanya na je, benki kuna hizo fedha? Lakini hakuna, hatuzioni," alisema Bashe.

"Mahali lilipofika hili jambo ni 'above' (juu) sisi Wizara ya Kilimo na ndiyo sababu nimeongea na Mkurugenzi wa TAKUKURU nikamwomba watu ili sisi tuwakabidhi tulichokifanya kutoka kwa JATU."

Alisema katika uchunguzi wao pia wamebaini JATU imefunga ofisi za Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro kwa madai kuwa wamehamia Mkoa wa Rukwa.

"Tuliwahoji JATU kuhusu yalipo mazao ya wakulima waliyowalimia wananchi wakadai yapo kwenye maghala, lakini timu ilizunguka siku saba kwenye mashamba na maghala kuangalia hawakukuta mazao hayo," alisema Bashe na kuongeza;

"Kwenye hili jambo ni vizuri sasa, 'tukahandover' (tukakabidhi) kila kitu kwa TAKUKURU, ili kufanyakazi yake na vyombo vingine vya ulinzi na usalama."

Bashe alisema tayari wamezungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni na kukubaliana azungumze na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillius Wambura na wanao husika na masuala ya fedha kutoka Benki Kuu (BoT), ili kuunda timu itakayofanyia kazi jambo hilo.

Aliwataka wakulima waliowekeza fedha zao kwenye kampuni ya JATU kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kufanya kazi yao na kukamilisha jambo hilo.

Alisema katika uchunguzi wao, walibaini kuwa fedha za wakulima Watanzania wanaoishi nje ya nchi walizotakiwa kulipwa msimu wa mazao 2019/20 na 2022/21 zilikuwa Sh. bilioni 4.066, lakini baada ya kupitia uhakiki wa taarifa za fedha za JATU za 2020, inaonekana kampuni hiyo ina Sh. milioni 230.

Alisema, hata hivyo baada ya uongozi wa kampuni hiyo kuhojiwa ulisema walikusanya Sh. bilioni 7.49 mwaka 2021.

Bashe alikemea mchezo wanaofanya JATU wa kuchukua fedha za wakulima na kuwaahidi kuwapa faida baada ya kulima, kuvuna na kupata faida.

Alisema yameanza kuibuka makundi mengine ya aina hiyo ambayo yanawalaghai wakulima, wanataka kuyaondoa kwa sababu yanawaondolea imani wawekezaji wenye imani ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo.

# Watoto waishio mazingira hatarishi walilia serikali

**Na Martha Sambo,** IRINGA

WATOTO wanaoishi mazingira hatarishi katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, wameililia serikali kuwaunganisha na fursa za kiuchumi ikiwamo vyuo vya ufundi ili wajikwamue kiuchumi badala ya kuishi na kufanya kazi hatarishi mtaani.

Kilio hicho wamekitoa wakati makarani wa sensa walipofika eneo la Mtaa wa Barabara Mbili mkoani humo, lenye watoto zaidi ya 30 wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.

Walisema licha ya kuwa na vipaji, wameishia kuwa ombaomba kwa kuishi mtaani kutokana na kukosa msaada.

Akizungumza na Nipashe muda mfubi baada ya kukamilisha zoezi la kuhesabiwa, kiongozi wa watoto hao ambaye naye ni mtoto (jina linahifadhiwa), alisema wameshiriki kikamilifu sensa ya watu na makazi ili serikali izitambue changamoto wanazokumbana, ikiwa ni pamoja na kukosa makazi na kujikuta wakiishi na kufanyakazi mtaani.

"Hatujui kama kweli serikali itatusaidia kutatua changamoto zetu, tuna vipaji vya kuimba, maigizo pamoja na ufundi, lakini hatuna mtu wa kutusaidia tumejikuta tukiishia kuokota makopo jalalani na kuyauza, ili kujipatia chakula kitu ambacho ni hatari kwetu, tunatamani tungepata fursa ya kusoma na kuendelezwa ili tuondokane na haya maisha," alisema kiongozi huyo wa watoto.

Ameelezea kuwako majanga mbalimbali yanayowakabili na kukosa msaada kutoka kwenye serikali za mitaa na kata kutokana na kutotambuliwa kama ilivyo kwa watoto wengine.

"Hatufanyi uhalifu, lakini mwisho wa siku tunajikuta tukiangukia mikononi mwa polisi na hatuna mtetezi, kupitia sensa hii niiombe serikali ituunganishe na vituo mbalimbali vya kulea watoto pamoja na kutupatia fursa ya elimu ili tusiwe tegemezi wala tusijihusishe na uhalifu," alisema.

Karani wa manispaa hiyo, Edger Edward alisema walikwenda wanapopatikana wenye mahitaji maalum na waliwatambua kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa.

"Tumeshirikiana na viongozi wa serikali za mitaa kuanzia wakati wa uhakiki hadi leo na tumeanza majira ya saa sita ili iwe rahisi kuwapata watoto walio mtaani kwani nao wana haki ya kuhesabiwa," alisema.

Karani katika mtaa wa Jumbe, Hidaya Jumbe, alisema licha ya mafanikio, kero wanazokutana nazo ni kukosa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wananchi hasa nyakati za usiku.

Kwa upande wake, Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi katika Manispaa ya Iringa, Raymond Nyenza, alisema tayari zoezi la sensa ya watu na makazi linaendelea katika maeneo mbalimbali na wameanza na makundi maalumu.

"Baadhi ya maeneo ambayo tumeanza nayo ni watoto wanaoishi katika mazingira magumu, nyumba za kulala wageni, Magereza, Polisi, hospitali na kwenye stendi ya mabasi na sasa bado zoezi hili linaendelea katika kaya mbalimbali," alisema Raymond.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Muhamed Moyo ni miongoni mwa viongozi walioshiriki zoezi hilo na kuwataka wananchi kushiriki kikamilifu kwa kutoa taarifa sahihi.

"Mimi tayari nimehesabiwa, niwaombe wananchi shirikini kikamilifu ili kurahisisha serikali kupata taarifa sahihi na takwimu kusaidia upangaji bajeti kulingana na uhitaji," alisema Moyo.

# Miaka mitano jela kujifanya mkurugenzi usalama wa taifa

**Na Mwandishi Wetu,** MLELE

MAHAKAMA ya Wilaya ya Iyonga Mlele, mkoani Katavi, imemuhukumu Raymond Bwire (28), kifungo cha miaka mitano jela, baada ya kukutwa na hatia ya kujifanya Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Mlele, Bilal Ahmed, alitoa hukumu hiyo juzi baada ya kesi namba 90 ya mwaka 2022 kusikilizwa mahakamani hapo na mshtakiwa kukutwa na hatia.

Kabla ya kusomwa hukumu hiyo, mwendesha mashtaka alidai kuwa Bwire ambaye ni mkazi wa Kamguluki Mkoa wa Mara, alikamatwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kutuma ujumbe mfupi kwenye simu ya mkononi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlele, Theresia Irafy, akimtaka kumsaidia mdogo wake kupata kazi ya utendaji wa kijiji kwa kujitambulisha kwa jina la Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa Bwire alitenda kosa hilo Agosti 12, mwaka huu, mkoani Mara.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akipokea barua za utambulisho za Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Ukimwi (UNAIDS), Martin Odiit katika Ofisi Ndogo za wizara jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PAC kuchambua hesabu za TRA, OSHA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIKAO vya baadhi ya Kamati za Bunge vinatarajiwa kuanza keshokutwa pamoja na mambo mengine zitafuatilia maazimio ya Bunge na kuchambua taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, kamati nne zitaanza vikao Agosti 25, mwaka huu ambazo ni Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), na Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Ratiba ya vikao hivyo inaonesha kuwa, PAC itaanza kuchambua hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usalama mahala pa kazi (OSHA).

Aidha, kamati zilizobaki zitaanza kukutana wiki ijayo huku shughuli zingine zitakazofanyika ni uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa mkutano wa saba wa Bunge.

Taarifa ya kitengo hicho ilisema, kamati za kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji.

Hata hivyo, Kamati ya PIC imepanga kupokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

"Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itapokea na kujadili taarifa za wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na za Wawakilishi wa Bunge la Tanzania katika vyama vinne vya kibunge."

"Kamati ya Bunge ya Bajeti imepanga kupokea na kujadili taarifa ya yatokanayo na kikao kilichofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Bunge kwa ajili ya majumuisho ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya matumizi ya wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2022/2023," ilisema taarifa ya kitengo hicho.

Vilevile, Kamati ya Bajeti itapokea taarifa zinazoiwezesha ufuatiliaji wa ukusanyaji na vyanzo vya mapato nchini.

## Maofisa wanaohodhi Viwanja kinyume cha sheria wapewa onyo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema serikali itawachukulia hatua kali ikiwamo kuwafukuza kazi maofisa ardhi kote nchini watakaobainika kuhodhi viwanja kinyume na sheria na pia watakaobainika kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi katika maeneo wanayofanyia kazi.

Alisema hayo juzi mjini hapo wakati wa kikao kazi na watumishi wa sekta ya ardhi wakiwamo wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Manispaa ya Morogoro, Ofisi ya Kamishna wa Ardhi pamoja na Chuo cha Ardhi.

Kikwete alisema wapo baadhi ya maofisa ardhi wanahodhi viwanja kinyume cha sheria huku wengine wakiwa sehemu ya migogoro ya ardhi.

Alisema maofisa ardhi wengine wanafanya vitendo vya ubabaishaji na kuifanya wizara hiyo kusemwa vibaya mbele ya wadau wakiwamo wananchi.

Kikwete alisema yeye na waziri wake wanawaahidi Watanzania kutokubali liendelee na kwa kukomesha vitendo viovu, wizara inatengeneza mfumo maalum wa kuondoa hoja zilizopo.

"Katika malalamiko yanayotajwa kwa wananchi huwa Ofisa Ardhi hakosekani, kama sio wa kwanza, wapili, watatu ndiyo maana tunaendelea kukumbushana, hata kama hapa nyie hamhusiki," alisema.

Aliwaonya kuacha kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi kwa kushindwa kusimamia na kutoa haki, au kushauri kulingana na uhalisia wa mipaka kuwa jukumu la wizara hiyo ni kupima, kupanga na kumilikisha ardhi kwa maendeleo na sio kutatua migogoro au kurasimisha ardhi ambako hufanyika baada ya matatizo.

Aliwahimiza maofisa hao kusimamia vizuri taaluma zao na mipango iliyokwishapangwa ikiwamo matumizi bora ya ardhi na kulinda mipango miji ambayo inategemewa kwa maendeleo.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Morogoro, Frank Mizikuntwe, aliiomba wizara hiyo kuangalia kero zinazowakabili ikiwamo uhaba wa watumishi wa ardhi hasa halmashauri za wilaya za Malinyi na Mlimba. Mizikuntwe alisema kwa sasa Wilaya ya Malinyi ina maofisa watatu pekee wanaohusika na ardhi akiwamo Ofisa Msaidizi wa Ardhi na msanifu majengo na haina mpima ramani wala ofisa mipango miji.

Aliishukuru wizara kupitia Katibu Mkuu kuahidi kuifanyia kazi ikiwamo uhaba wa vitendea kazi, ambayo tayari zimeletwa kompyuta tano.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro, Huruma Lugala, alisema kutokana na changamoto ya ukusanyaji wa madeni yatokanayo na upimaji waliomba wizara iingilie kati ili fedha hizo zaidi ya Sh. bilioni 4.4 zisaidie utatuzi wa changamoto.

Alisema licha ya uhaba wa watumishi, upungufu wa vifaa vya kufundishia, uchakavu wa miundombinu, tatizo la ukusanyaji wa madeni na ukosefu wa bodi ya ushauri tangu Desemba mwaka jana, jambo linaloathiri utoaji wa matokeo ya mitihani ya wanafunzi na kushindwa kufanyika mkataba kati ya chuo na Hazina.

## HABARI KITAIFA



Wachuuzi wa matunda wakinunua machenza katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kwenda kuyauza mitaani. Chenza moja liliuzwa 60/- kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zaidi ya wanafunzi 80 walala ndani ya darasa

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** TABORA

WANAFUNZI 85 wa Shule ya Sekondari ya Nanga, Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, wanalala kwenye chumba cha darasa kutokana na paa la bweni lao kuezuliwa na mvua zilizonyesha Novemba, mwaka jana.

Mkuu wa Mkoa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, alieleza hayo kwa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, alipokuwa anafanya ukaguzi wa jengo la afya.

Alisema eneo la Nanga walipata tatizo la mvua ya upepo ambayo ilisababisha madhara makubwa, ikiwamo kituo cha afya kuathirika, nyumba ya wauguzi na Shule ya Nanga Sekondari.

"Bwalo la kulia watoto mpaka leo halina paa na bweni la watoto wa kiume kwa sasa hivi wanalala madarasani mimi nilitoa mabati 100 niliongea na Red Cross waliniunga mkono na kutoa mabati 100 na kuwapa mkono wale wote walioathirika wakaweza kupata magodoro na vitu mbalimbali vya kuendelea na maisha," alisema.

Dk. Buriani alisema awali wanafunzi 120 walikuwa wanalala darasani na awamu ya sasa waliochaguliwa kuingia kidato cha tano wamechukuliwa wachache, kwa sasa wanaolala kwenye chumba cha darasa ni 85.

"Imetulazimu kuchukua darasa moja ambalo lilikuwa tupu tufanye kama bweni tukahamishia vitanda," alisema.

Aliomba msaada na tayari waliandika barua kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa ili kusaidiwa ujenzi wanafunzi warudi kwenye bweni badala ya kulala darasani.

Aidha, alisema kwa mkoa wa Tabora kwa ujumla wanamshukuru Raisa Samia Suluhu Hassan, kwa mambo mbalimbali ya maendeleo aliyowafanyia.

Alisema walikuwa na shida ya maji walipatiwa fedha zaidi ya Sh. bilioni 148 ili kutoa maji Ziwa Victoria na kuyasambaza katika wilaya za Igunga, Urambo, Sikonge na Kaliua.

Shaka kwa upande wake alisema maombi yote yaliyotolewa ya kutaka yaende kwa Rais Samia Suluhu Hassan atayafikisha kama yalivyowasilishwa ili kero hizo zitatuliwe.

"Hawa wabunge watatupa vizuri kwa maandishi ili yaende kwa uhakika sambamba na changamoto ya mapato ya stendi atakwenda kuzungumza na waziri ili kushauriana namna bora ya kulinda mapato hayo na halmashauri zetu zisiporomoke katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu," alisema Shaka.

Kadhalika, alisema wanachokiangalia ni fedha za miradi ya maendeleo ambazo zinaletwa na Rais Samia, zinakwenda kutafsiri dhana yake, maono na nia yake ya kupunguza kero kwa wananchi.

Alisema ukiangalia aina ya ujenzi na thamani halisi ya fedha iliyotumika unaona namna ambavyo wamekuwa waungwana na kuheshimu fedha zinazoletwa na Rais.

# Wananchi waridhia ongezeko bei maji

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WANANCHI katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, wameridhia ombi la kurekebisha bei za huduma za maji lililotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA).

Wananchi hao wameridhia ombi hilo katika kikao maalum kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea kilichoshirikisha wawakilishi kutoka makundi yote wakiwamo wananchi, madiwani na wenyeviti wa mitaa.

Licha ya kuunga mkono mapendekezo ya kurekebisha bei za maji, wananchi hao wameiomba SOUWASA kuboresha miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na kuongeza saa za wateja kupata maji.

"Tunaunga mkono marekebisho ya bei za huduma za maji, lakini tunaomba ongezeko hilo liende sambamba na kuboresha huduma zenu SOUWASA. Tunapendekeza matumizi ya LUKU kwenye maji ili kupunguza malalamiko kwa wasoma mita na kuongeza mtandao wa majitaka mjini Songea," alisema Mathew Ngalimanayo, Diwani wa Mjini, Manispaa ya Songea.

Akizungumza wakati anafungua na kufunga kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, aliwapongeza wananchi wa Manispaa ya Songea kwa kujitokeza kwa wingi katika kikao hicho na kuridhia mapendekezo ya kurekebisha bei za huduma za maji.

Kanali Thomas alisisitiza kuwa maji ni huduma nyeti kwa ustawi wa wananchi na uchumi na kwamba upatikanaji wa majisafi na ya kutosha ni kielelezo cha ubora wa maisha ya watu.

"Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kufanya mabadiliko na maboresho makubwa katika sekta ya maji," alisema .

Pia alisema serikali imeongeza wawekezaji katika sekta ya maji ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo ili kufikia lengo la asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025.

Mkurugenzi Mtendaji wa SOUWASA, Mhandisi Patrick Kibasa, amesema hadi sasa mamlaka yake imetoa maji safi kwa asilimia 86 na kwamba ina mtandao wa kusambaza maji safi wenye urefu wa kilometa 522.5 na wateja 20,266 wameunganishwa katika mtandao wa majisafi.

Kibasa aliyataja malengo ya SOUWASA kuwa ni kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 86 hadi asilimia 95 mwaka 2025 na kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 22 hadi asilimia 20 ifikapo mwaka huo.

Mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Richard Kayombo, aliwapongeza wadau wa Songea kutoka makundi yote kushiriki kikamilifu katika kikao hicho na kuunga mkono hoja ya kurekebisha bei za huduma za maji.

"Wananchi waliopata fursa ya kuzungumza kwenye kikao hiki shida yao si gharama ya maji. Wanachohitaji ni upatikanaji wa majisafi katika maeneo yao ili kuondoa kero ya maji." Alisema.


UN WOMEN

United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

## CALL FOR PROPOSALS

The United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women (UN Women) Tanzania is pleased to announce a Call for Proposals from organizations with a track record in human rights, women's rights and gender equality to implement creative and innovative strategies, approaches, and interventions to transform gender norms, discriminatory behaviour and practices to promote women and girls' voices, meaningful participation, leadership, and economic rights at the local level (ward, village, streets, vitongoji, e.t.c) in the selected district councils of Dar es Salaam, Coast, Lindi, Mtwara , Arusha and Singida.

The organizations should have a base and previous experience in implementing projects in the respective regions. If it's a national organization that does not have experience in the respective regions, but plans to expand its projects to the WLER Project regions building on learnings from the implantation of similar projects, it should indicate previous collaboration with other human and women's rights organizations and networks including those promoting the rights of young women and women with disabilities; and duty bearers, including local government actors and community facilitators in the respective regions to deliver on the project objectives. The organizations should also demonstrate experience working with opinion makers such as community and traditional leaders, religious leaders, male gender equality and women's empowerment champions, decision-makers, and the media.

The full Call for Proposal (CFP) may be downloaded from:

https://www.unwomen.org/en/about-us/programme-implementation/2022/08/call-for-proposals-unw-esa-tza-2022-001-transforming-gender-norms

The Call for Proposals will be open until **31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT) (Tanzanian Time).**

**All proposal MUST be submitted through email cfp.tanzania@unwomen.org with subject line REF: CFP No. UNW-ESA-TZA-2022- 001 on Transforming Gender norms and discriminatory behaviours and practices at local levels to promote women and girls' voices, meaningful participation, and leadership.**

Only **those short listed** will be contacted for further screening and consideration.

**Proposals received after the deadline will not be considered.**

**For more information, please email: agness.hanti@unwomen.org by 31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT)**

217003101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha watoto wanaoishi mazingira hatarishi kisikilizwe

**WATOTO** wanaoishi mazingira hatarishi juzi walitoa kilio kwa makarani wa sensa walioanza kufanya zoezi la kuwahesabu usiku wa kuamkia jana, wakiiomba serikali kuwaunganisha na fursa za kiuchumi ikiwamo vyuo vya ufundi ili waondokane na mazingira ya kuishi na kufanya kazi hatarishi mtaani.

Kilio hicho cha watoto kinaonesha umuhimu wa sensa ya watu na makazi kufanyika ili kupata takwimu sahihi za watu wa rika zote kwa maendeleo yao.

Watoto hao zaidi ya 30 waliohesabiwa Manispaa ya Iringa, ni kielelezo cha wenzao wanaoishi katika mikoa tofauti kwenye mazingira hayo hatarishi.

Kilio chao kikubwa ni kuwa licha ya kuwa na vipaji, lakini bado wameishia kuwa ombaomba na kuishi mtaani kutokana na kukosa msaada.

Hamasa iliyokuwa ikitolewa ya kuwataka wananchi wote kushiriki sensa ya watu na makazi, bila kujali wanaishi katika mazingira gani, imewahamasisha watoto hao kujitoa kushiriki kuhesabiwa baada ya kujua umuhimu wake.

Wameamua kushiriki kikamilifu zoezi la sensa ya watu na makazi ili serikali izitambue kero wanazokumbana, ikiwa ni pamoja na kukosa makazi na kujikuta wakiishi na kufanyakazi mtaani.

Matumaini yao ni kuona serikali inawasaidia kutatua kero zao kwasababu wamesema wana vipaji vya kuimba, maigizo pamoja na ufundi, lakini wanakosa mtu wa kuwasaidia na kuishia kuokota makopo jalalani na kuyauza ili kujipatia chakula kitu ambacho ni hatari kwao.

Wanatamani kupata fursa ya kusoma na kuendelezwa ili waondokane na maisha hayo ambayo wakati mwingine huwaletea misukosuko ya kupigwa na kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Katika kilio chao wanasema wanakutana na majanga mbalimbali, lakini wanakosa msaada kutoka mamlaka kama serikali za mitaa na kata kutokana na kutotambuliwa kama wanavyotambuliwa watoto wengine.

Watoto wanaoishi katika mazingira hayo, baadhi yao hawakupenda kuishi hivyo, lakini kutokana na shida mbalimbali zinazotokea hujikuta wakiingia katika mazingira hayo.

Mara nyingi watu huwaona kama wahalifu kutokana na mwonekano wao na makundi wanayoambatana nao na wakati mwingine wakijikuta wakiangukia mikononi mwa polisi kwa kukosa mtetezi.

Kupitia sensa matarajio yao ni serikali kuwaunganisha na vituo mbalimbali vya kulea watoto pamoja na kuwapatia fursa ya elimu ili wasiwe tegemezi au kujihusisha na uhalifu.


Kupitia sensa ni matumaini yetu idadi yao itasaidia serikali kuwatambua na hatimaye nao kupata haki zao za msingi kama watoto wengine wanaopata malezi ya wazazi wao.

Kazi iliyofanywa na viongozi wa serikali za mitaa kuanzia wakati uhakiki hadi siku ya sensa imesaidia makarani kuwapata kwa urahisi watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kufanikisha zoezi hilo liende kama lilivyopangwa.

Elimu iliyotolewa imesaidia wananchi wengi kuelewa umuhimu wa kushiriki zoezi la kuhesabiwa kwa kuwa wanatambua bila serikali kujua idadi ya watu ilio nao haiwezi kupanga mipango ya maendeleo kwa ufanisi.

Nia ni kuwezesha wananchi wote kufaidika na mipango ya maendeleo iliyowekwa na serikali kuanzia kwenye afya, elimu na huduma zote muhimu ikiwamo majengo bora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Katiba mpya ikamalize utata usawa kijinsia

**USAWA** wa kijinsia unalenga kuhakikisha uwepo wa haki za binadamu kwa wanawake na wanaume ili washiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya taifa lao.

Halikadhalika kwa kuyaangalia makundi dhaifu kwenye uongozi yanayowekwa pembeni wakiwamo wanawake ili kuwawezesha na kuwapa nafasi kwenye kushiriki majukumu ya kuendeleza jamii zao.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, haki za binadamu ambaye ni mtafiti wa mambo ya maendeleo ya jamii, Deus Kibamba, anashauri kuwa usawa wa kijinsia uzingatiwe pale panapofanyika uteuzi wa aina yoyote ili kuyapa makundi yote wanawake, wanaume, wenye ulemavu na vijana nafasi.

Anashauri kuwa katika nafasi za kuchaguliwa kuna maeneo wanazingatia usawa wa kijinsia na kwamba yote yatatimia iwapo katiba itaandikwa upya na ikitamka na kueleza maeneo ambayo ni lazima kuwepo na usawa huo katika uteuzi na kupendekeza hatua za kuchukuliwa kwa watakaopuuza.

Anasema katiba ina umuhimu wa kuainisha maeneo unapohitajika usawa kwa sababu bungeni leo, idadi ya wanawake ni asilimia 39, viti maalumu asilimia 9, madiwani wakuchaguliwa Tanzania Bara ni asilimia 7 na wanawake waliochaguliwa kwenye serikali za mitaa ni asilimia 2.6.

Ikiwa hali ndiyo hiyo kwa wanawake katika nafasi za kuchaguliwa ukweli ni kuwa ni wachache na kumekuwa na changamoto zinazosababisha hata masuala ya wanawake yasifanyiwe kazi hasa huduma za kijamii.

Ni ukweli kuwa zipo sehemu ambazo mamlaka na uongozi wenye usawa kati ya wanawake na wanaume unapatikana lakini sehemu nyingine wanawake wanakosekana.

Ndiyo maana kuwapo na vigezo ambavyo vitaonyesha kipi cha kuzingatiwa kwenye katiba ili kuwa na usawa wa kijinsia ni suala lisilokwepeka wakati huu wa kuandaa katiba mpya inayotegemewa kubeba maoni mbalimbali ya Watanzania wa jinsia zote.

Ni vyema pia kuwa na kampeni ya kuchagiza mamlaka zinazoteua ziwekewe vigezo na masharti ili kuwepo usawa katika kuwateua viongozi kiusawa. Wanawake wakitakiwa kuteuliwa kwa ulinganifu au uwiano sawa sawa na ule wa wanaume bila kuwasahau wenye ulemavu, vijana na makundi kama hayo.

Takwimu zinazotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi zinaonyesha kuwa kipindi cha mwaka 2018 uteuzi uliofanywa na awamu ya tano ulifikia wateuliwa 463 na kati yao wanawake walikuwa 37 sawa na asilimia 7.0 huku wanaume walioteuliwa wakiwa 426 sawa na asilimia 92.01.

Liliana anaeleza kuwa uteuzi huo unaibua hisia kuwa hizo hisani za kiongozi aliyepo madarakani kwa wale anaowapa majukumu, kinachotakiwa ni kuwepo sheria ambayo itaelekeza kuwepo na usawa katika kuwateua watendaji na viongozi na kila atakayeingia madarakani afuate utaratibu huo ili kuendeleza usawa wa kijinsia.

Ili kuondoa fikra hizo yote hayo yatafanikiwa iwapo Tanzania itaandaa katiba mpya ambayo itabeba mambo mengi ya kuzingatia usawa, kuanzia kwenye ulingo wa siasa, uongozi wa taasisi za umma na binafsi.

Ukiañgalia katika vyama vya siasa uteuzi wa wagombea, viongozi na wawakilishi mbalimbali unajaa ukakasi kwa kuwa ni kioo cha mfumo dume ambao bado inatamalaki katika nafasi za juu za uchaguzi wa viongozi.

Anasema sheria za vyama vya siasa zinawataka kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia, lakini ni vichache vina katiba zinazozingatia suala hilo na vingine vingi vinaendeleza mfumo dume, hivyo dawa ni katiba na si vinginevyo.

Vyama vya siasa ifike wakati viachane na mfumo dume kutokana na ukweli kuwa mchango wa kila mmoja awe mwanamke, wanaume mwenye ulemavu, kijana na raia yeyote mchango wake unahitajika kwenye maendeleo ya taifa.

Yote hayo yanawapa wabunge jukumu la kuwaletea Watanzania mabadiliko ya kisheria, kisera, miongozo ili kuwa na Tanzania yenye usawa na inayoshirikisha wadau na raia wake wote bila kujali changamoto za kimaumbile wala jinsi zao.



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, akizungumza na viongozi wa dini mbalimbali wa mkoa huo jana, alipokuwa akiwahamasisha katika hatua ya mwisho ya kuhakikisha watu wanashiriki kwenye sensa ya watu na makazi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ubovu stendi wakosesha halmashauri mapato

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba limelalamikia ubovu wa stendi ya mabasi ya Kemondo hatua ambayo wameeleza kuwa inasababisha mamlaka hiyo kukosa mapato.

Kutokana na hali hiyo, wamemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kutafuta fungu kwa ajili ya kukarabati kituo hicho na kuhamisha kituo cha magari cha Kyema, ili vituo hivyo vianze kufanya kazi na kuingiza mapato kama ilivyokusudiwa.

Akizungumza katika Baraza la Nne la kufunga mwaka wa fedha 2021/22, Mwenyekiti wa Halmashauri, Pius Ngeze, alisema kwa sasa hawapati ushuru wowote kutoka katika vituo hivyo baada ya wahusika kugoma kulipa wakidai kanuni haziruhusu kutozwa ushuru barabarani.

"Stendi ina hali mbaya, magari hayaingii na madereva wanagoma kwamba hawawezi kulipishwa ushuru wakiwa barabarani, kwa hiyo pakarabatiwe pawe na hali nzuri ili magari yaingie na ushuru uanze kutozwa kama kawaida kwa sababu hali hii inasababisha kupoteza mapato ya halmashauri," alisema Ngeze.

Alisema kituo hicho cha Kemondo ambacho kiko katika barabara kuu inayotoka Bukoba kwenda mikoani na nchi jirani, kinapaswa kukamilika ndani ya mwezi mmoja kuanzia juzi ili kianze kupokea magari na ushuru uanze kutozwa.

Kuhusu kituo cha Kyema, alisema kihamishwe eneo kilipo na kupelekwa katika eneo lililoko jirani na eneo hilo na kwamba kama halmashauri haina eneo basi ianze kufanya mazungumzo na wananchi wenye yale ili waone ni namna gani wanaweza kufidiana na kujenga kituo cha magari.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Fatna Laay, alisema zimeshatengwa Sh. milioni 1,00 kwa ajili ya kukarabati stendi ya Kemondo na kwamba Sh. milioni 50 tayari zimetolewa ili kazi iendelee.

Naye Diwani wa Kemondo kilipo kituo hicho, Alhaji Atwib Mussa, alisema kituo hicho ni chanzo kizuri cha mapato kwa halmashauri na kushauri ukarabati ufanyike haraka. Pia alipendekeza kituo cha zamani cha magari kilichoko Kemondo Centre kifungwe na magari yaziuwe kupakia na kushusha abiria katika eneo hilo, ndipo kituo kipya kitafanya kazi kwa ufanisi.

# Jamii yatakiwa kujenga tabia kuripoti polisi matukio ukatili

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro limeitaka jamii kujenga tabia ya kuripoti matukio ya mimba za utotoni yanayojitokeza badala ya kumalizana majumbani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro Fortunatus Musilim, alitoa rai hiyo jana wakati akielezea matukio ya mimba za utotoni mkoani humo kuonekana kupungua kutoka mimba 92 mwaka 2019/20 hadi 61 mwaka 2020/21.

Alisema kupungua kwa matukio hayo kumetokana na jitihada za elimu zinazofanywa na dawati la jinsia la polisi, lakini matukio hayo ni yale yaliyoripotiwa polisi pekee.

Alifafanua kuwa matukio yaliyotokea mwaka 2019/20 ni kutoka katika wilaya za Morogoro (20), Kilosa (13), Kilombero (4), Ruhembe (8), Malinyi (2), Ulanga (2), Mvomero (13) na Gairo (30).

Alisema matukio yaliyotokea mwaka 2020/21 kutoka katika wilaya za Morogoro (12), Kilosa (10), Kilombero (5), Malinyi (1), Ulanga (3), Mvomero (9) na Gairo (21).

Matukio 44 kati ya hayo yalifikishwa mahakamani huku matukio 67 yapo kwenye upelelezi na 11 yalifungwa kutokana na kukosa maelezo ya kujitosheleza.

Hata hivyo, alisema matukio mawili kati ya hayo yalibainika kuwa hayana makosa kamili ya kuendelea kusikilizwa wakati matukio 26 tayari yameshapatiwa hukumu mahakamani.

Kamanda Musilim aliitaka jamii kuendelea kutoa ushirikiano na Jeshi la Polisi kwa kupinga vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto ili kuhakikisha vinapungua au kuisha kabisa.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema suala la mimba za utotoni hutokea kwa sababu ya changamoto kubwa ni malezi ya upande mmoja kwa mama pekee na baba kukosekana nyumbani, vishawishi kwa madereva wa bajaji na bodaboda kutokana na tatizo la usafiri.

"Watoto wenyewe wamesema nilipowahoji kwamba mara nyingi wanaambiwa 'kabla hujaenda shule pitia kwangu' nao wanapitia na kupewa kiasi cha pesa, shilingi elfu mbili, shilingi elfu tatu, hushawishiwa na kuingia katika mapenzi wakiwa wenye umri mdogo," alisema.

Alisema wilaya itatoa elimu ya kutosha kwa watoto kupitia klabu zinazoundwa kwenye shule za sekondari ili kuwajengea uwezo wa kuepukana na vishawishi na kuona viashiria mapema vya mtoto kutumbukia kwenye suala la mapenzi katika umri mdogo usiostahiki.

Alipongeza mpango wa kurudisha watoto shuleni wanapopata mimba na kwamba hiyo itasaidia kuondoa adhabu mbili kwa mtoto kuwa amepata mimba na kukosa masomo.

Miezi mitatu iliyopita wanafunzi sita wa shule moja ya sekondari Mafiga Manispaa ya Morogoro baada ya vipimo waligundulika kuwa na ujauzito na kusimamishwa shule.


## UBALOZI WA MAREKANI, FINLAND NA WATAALAM MBALI MBALI DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani, Finland na wataalam mbali mbaliwatauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani na Magari **tarehe 27 August, 2022 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00asubuhi:Sofa set, Chest drawer, Dining table, chairs, Book case, Drasser, Meza za ofisi, Viti, Vitanda, Makabati, Fridge double door, Deep Freezer, Washer, Majiko ya umeme, Gas, Garden Table, Computer set, TV Set, Kyosera Photo copy m/c model 5500ina vingine vingi.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Scania Truck Tanker 9,000 Liters | P250 - Diesel Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 1 | Land Rover Freelander Station Wagon | SALFA -Petrol Engine | 2010 | Haujalipwa |
| 1 | Ford Ecosport Station Wagon | FY58 - Petrol Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Murano Station Wagon | Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | ZD30 Diesel Engine | 2015 | Umelipwa |
| 1 | Tata Pick -up 2Tons | Mobile 207 Diesel | 2008 | Umelipwa |
| 2 | Wheel Loader 0.25 Cubic Meter | 16.2KW Diesel Engine | 2014 | Umelipwa |
| 1 | Podium Trailer 3 Tons | Single Exel | - | Umelipwa |
| 1 | Catic Tiper Tuck 3Tons | LNJ-Diesel Engine | 2007 | Umelipwa |
| 1 | Suzuki Motorcycle | TF 125 | 1995 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 24 mpaka 26 August, 2022, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 1 September, 2022 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Garilitauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu lazima awe na bid namba itakayopatikana getini.
7. Kila mtu atatakiwa kuchukua tahadhari ya Corona kwa kuvaa Barakoa na kuzingatia umbali

**Kwa maelezo zaidi waone:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA** **DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

217008901

# Mstaafu alia halmashauri kuchukua shamba lake

**Na Mohab Domonic,**
KAHAMA

MKAZI wa Kijiji cha Kakola, Kahama mkoani Shinyanga, Benson Munuo, ameilalamikia Halmashauri ya Msalala kwa kupima shamba lake lenye ukubwa wa ekari 15 na kupimwa viwanja vya makazi bila kushirikishwa.

Pia Munuo amegoma kupokea Sh. milioni 20 alizotakiwa kulipwa kama fidia ya eneo lake.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi kijijini kwake hapo, Munuo alisema halmashauri imechukua uamuzi huo bila kumshirikisha na kwamba anapinga kitendo cha shamba lake kupimwa pasipo makubaliano wala kuhusishwa na amegoma kupokea fidia kwa sababu hazilingani na gharama ya mali zilizomo kwenye shamba hilo.

Munuo alisema shamba hilo lililoko Kitongoji cha Nyangaka, Kata ya Bugarama, limepimwa viwanja vya makazi wakati alishaliendeleza na lina rasilimali ambazo ni mabwawa matatu anayofuga samaki, miti mbalimbali ya mbao na ya matunda zaidi ya 1,000.

Alizitaja mali zingine kuwa ni mazao ya chakula, migomba, mihogo, miwa, mitikiti, mapalachichi, katani na mizinga ya nyuki. Mzee Munuo alisema upimaji uliofanywa wa viwanja vya makazi na kuwekwa alama za vigingi, hautambui kwa sababu hakushirikishwa, hivyo kuomba taratibu zifaatwe kwa mujibu wa sheria ya ardhi.

Jirani wa Munuo, Issa Ibrahim, alisema eneo hilo aliloliendeleza kwa miaka 11 alilinunua mwaka 2007 baada ya kustaafu kazi katika mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu na kuamua kuwekeza hapo kwa shughuli zake za kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula, kupanda miti ya matunda na mbao, ufugaji wa samaki na nyuki na kuomba atendewe haki.

Naye Mtema Nkamba, jirani wa mlalamikaji huyo, alisema Munuo hajawahi kushirikishwa juu ya upimaji wa shamba lake na toka lipimwe watu wasiofahamika wamelivamia na kuanza kuvuna miti na mazao yake ya chakula pamoja na kuchoma moto eneo hilo na kumsababishia hasara.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyangaka, Pili Msomi, alipoulizwa alisema kabla ya upimaji huo kufanyika waliitisha mkutano wa hadhara juu ya suala hilo lakini Munuo hakuhudhuria hali iliyozusha malalamiko hayo baada ya halmashauri kufanya kazi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala, Edward Fussi, alipoulizwa alikiri kuwapo kwa upimaji wa maeneo mbalimbali katika halmashauri yake baada ya serikali kuwapatia Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya kazi hiyo pamoja na kulipa fidia na kumtaka yeyote mwenye malalamiko kufika ofisini kwake.



Spika wa Bunge, Tulia Ackson (wa pili kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya Mwanga Hakika, Mhandisi Ridhiwani Mringo (katikati), akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Mwanga Hakika, Jagjit Singh (wa pili kushoto) na Mwenyekiti Msaidizi wa Bodi ya benki hiyo, Raymond Thadeus (kushoto), katika hafla ya kuifanya benki hiyo kuwa ya biashara, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja ABC kunufaika na mikopo kupitia mishahara

**Na Joseph Mwendapole**

WATEJA wa Benki ya Biashara ya Akiba (ACB), sasa watanufaika na mikopo ya chapchap kupitia mishahara (Salary Advance) kwa ajili ya dharura na fursa zinazojitokeza papo kwa papo.

Meneja Mwandamizi wa Idara ya Biashara, Emmanuel Mseti, alisema mapema wiki hii kuwa wateja wa benki hiyo pia watanufaika kwa kupata huduma mbalimbali zilizounganishwa na akaunti zao.

Alitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na mikopo ya wafanyakazi, mikopo ya nyumba kwa ajili ya dharura na fursa zinazojitokeza papo kwa papo.

"Huduma hii inapatikana ndani ya muda mfupi iwezekanavyo kutokana na uharaka wa mteja katika kufanikisha taratibu zinazohitajika na huduma hii inaweza kupatikana ndani ya saa 24," alisema.

Pia alisema katika kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja wake, ACB inafanya jitihada kuboresha huduma na bidhaa mbalimbali kuendana na mahitaji ya wateja na soko kwa ujumla.

Mseti alisema ACB imefanya maboresho kwenye utoaji huduma kwa wateja wake kwenye nyanja mbalimbali hasa upande wa wateja binafsi. Aliongeza kuwa muda wa marejesho wa mikopo ya nyumba umeongezwa kufikia miezi 84 au miaka 7 kwa ajili ya kuleta unafuu kwa mkopaji katika kumudu marejesho. Vile vile alisema mikopo hiyo ya nyumba ijulikanayo kama Akiba Mortgage Loan inatolewa kwa ajili ya kununua nyumba, kujenga nyumba, kumalizia ujenzi pamoja na kufanya marekebisho ya nyumba.

Aidha, Mseti alisema benki hiyo pia inatoa huduma ya mikopo inayodhaminiwa na hati fungani za serikali kwa watu walioajiriwa na wasioajiriwa na hati fungani itasimama kama dhamana ya kupata mkopo.

Mseti pia alisema 'Akiba Salary; ina gharama nafuu za uendeshaji na akaunti hiyo pia imeunganishwa na huduma za kidijitali kama Akiba Mobile zinazoleta urahisi zaidi kwa mteja katika kupata mahitaji ya kibenki.

Alisema ACB inaendelea kuboresha huduma zake pamoja na kuanzisha nyingine nyingi mpya ili iweze kuwahudumia Watanzania wote na wafanya biashara kuanzia wa tabaka la chini, kati na wa juu hususan kampuni kubwa na taasisi mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mseti, mbali na kuwa na matawi sehemu mbalimbali, benki pia ina zaidi ya mawakala 1,500 nchi nzima kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja.

## Walaani mzee kuzikwa yu hai

**Na Halfani Chusi**

BARAZA la Wazee la Taifa (BWZT), kwa kushirikiana na mtandao wa mashirika yanayotetea haki za wazee nchini ikiwamo Shirika la HelpAge International Tanzania, limeeleza kusikitishwa na wananchi wanaodaiwa kumzika Mzee John Komba (78), akiwa hai na kumsababishia kifo.

Tukio hilo lilitokea juzi Kijiji cha Mahanje, Madaba mkoani Ruvuma, baada ya wananchi kushirikiana na baadhi ya wanafamilia kumwadhibu mzee huyo kwa madai ya kuhusika kwenye mauaji ya binti yake, Severine Komba (34).

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na baraza hilo na mashirika ya kutetea haki za wazee, kitendo hicho ni kinyume cha sheria na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa, Lameck Sendo, alisema tukio hilo ni mwendelezo wa matukio ya kinyama wanayofanyiwa wazee kutokana na imani potofu ya dhana za kishirikina.

"Tumepokea kwa masikitiko tukio la mauaji ya Mzee Komba, inasemekana kimefanywa na baadhi ya wananchi wenye hasira kali kwa kushirikiana na baadhi ya wanafamilia wakati wakiwa kwenye mazishi ya mtoto wake Severine Komba, wakimtuhumu mzee huyo kuwa alihusika katika mauaji ya mwanawe,"alisema.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Mashirika ya Wazee Tanzania, Coltilda Kokupima, aliwataka wananchi kuacha kuchukua sheria mkononi.

"Kitendo alichofanyiwa marehemu Mzee John Komba, ni kuvunja sheria za nchi, kuvunja katiba ya nchi, pamoja na kwenda kinyume na imani zetu za dini kwa hiyo ifike mahali watu watambue kuwa uzee ni hatua katika ukuaji hivyo hata wao itafika wakati watazeeka," alisema.

"Wazee hawa mnaowatuhumu leo kuwa ni wachawi mkumbuke kuwa ndio waliwalea na kuwatunza mpaka hapo mlipofika kwa hiyo tunaomba wazee waheshimiwe, wathaminiwe, badala ya kubezwa, kudharauliwa na hata kuuwawa kama tukio hili lilivyotokea," alionya.

Mkurugenzi wa Shirika la HelpAge Tanzania, Smart Daniel, aliwataka wananchi pamoja na viongozi wa ngazi zote za serikali kukemea vitendo hivyo pamoja na kutoa taarifa wanapobaini uwepo wa matukio ya aina hiyo.

"Tukio hili linatukumbusha tukio jingine kama hilo lililotokea mkoani Singida, katika Kijiji cha Kisharita wilayani Iramba, ambapo wazee watatu wa kike waliuawa siku moja kwa kutuhumiwa eti ni wachawi.

Lakini kipekee tunaupongeza uongozi wa Wilaya ya Songea akiwamo Mkuu wa Wilaya na kamati yake ya ulinzi na usalama, kwa hatua za haraka walizozichukua ikiwamo kuwabaini na kuwakamata washukiwa wa tukio hili kwa hiyo nilikuwa napendekeza tuongozwe na kauli mbiu isemayo 'Uzee na kuzeeka haukwepeki' hivyo kila mtu atakaye bahatika kuishi miaka mingi lazima atazeeka."

HABARI KITAIFA

## Benki ya Dunia yatoa bil. 17/- huduma mama na mtoto

**Na Yasmine Protace**

BENKI ya Dunia (WB) imetoa msaada wa Sh. bilioni 17 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya mama na mtoto.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo wakati alipokutana na wadau kutoka Shirika la Global Financing Facility (GFF) kutoka Benki ya Dunia, ambao wamefadhili mradi wa kitita cha uzazi salama katika Hospitali ya Rufani ya Bombo, mkoani Tanga.

Alisema fedha hizo zinatarajiwa kutumika katika ununuzi wa vifaa, kuwajengea uwezo watumishi wa afya ili kubaini tatizo linalomkabili mjamzito katika hatua ya awali na kudhibiti mapema.

"Wadau wa (GFF) wamefadhili huduma ya mama na mtoto katika mikoa mitano hapa nchini na tayari matokeo ya awali yameonesha kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kwa asilimia 50 na asilimia 25 ya vifo vitokanavyo na uzazi," alisema.

Kadhalika, alisema utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa kushirikiana na Hospitali ya Lutheran ya Hydom iliyoko mkoni Manyara.

"Dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuokoa maisha ya watoto wachanga pamoja na mama wajawazito," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Mama na Mtoto, Dk. Ahmad Makuwani, amesema lengo la utekelezaji wa mradi huo ni kuhakikisha wajawazito na watoto wachanga wanakuwa na maisha bora nchini.

"Vifo vya mama mjamzito na watoto wachanga kwa Tanzania bado ni janga kubwa hivyo bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunazidi kupunguza vifo hivi nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji kutoka Hospitali ya Hyidom, Dk. Paschal Mdoe, alimshukuru Waziri Ummy kwa ushirikiano alio utoa kwa hospitali hiyo kutekeleza mradi huo katika mikoa mitano na kuleta matokeo chanya.

# 'Mashindano ya madereva kuwahi bonasi chanzo cha ajali'

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MABASI yanayofanya safari kati ya Mwanza, Singida, Dodoma na Dar es Salaam yamedaiwa madereva wake kushindana kwenda mwendo wa kasi ili kuwahi kufika mapema kwa kuchochewa na bonasi inayodaiwa kutolewa na matajiri wa magari hayo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Mkoa wa Singida, Prisca Maleta, alifichua siri hiyo wakati wa mazishi ya Diwani Viti Maalum wa Tarafa ya Kinampanda wilayani Iramba, Winjuka Mkumbo, ambaye alikuwa ni miongoni mwa watu sita waliopoteza maisha kwa ajali ya basi la kampuni ya Tanzanite.

Ajali hiyo iliyohusisha basi lenye namba za usajili T 916 DNU ilitokea Agosti 17, mwaka huu saa 9:30 alasiri katika Kijiji cha Mbwasa, wilayani Manyoni, Barabara Kuu ya Singida-Dodoma na kusababisha vifo vya watu watano akiwamo diwani huyo.

Maleta ni shuhuda wa kwanza wa ajali hiyo aliyetoa msaada kwa majeruhi na kuzisitiri maiti, aliwaeleza waombolezaji kuwa mabasi yamekuwa yakishindana kwenda mwendo kasi kuwahi bonansi inayotolewa na matajiri wa mabasi.

"Tunaomba serikali kuliangalia jambo ili kwani matajiri wengi wanawapatia madereva wao minara (bonansi) wa kwanza kufika ndiye atakayepewa bonasi na suala la pili ni wale watu wanaofika eneo la ajali tukiwaamini kwa asilimia 100 ndiyo wanakuwa wa kwanza kuwafilisi kwa kuwaibia majeruhi," alisema.

Alisema baada ya ajali kutokea aliongea na marehemu (Winjuka) eneo la ajali na kumweleza kuwa chanzo cha ajili ilikuwa mwendo wa basi hilo tangu linaondoka Singida.

Kabla mauti hayajamkuta diwani huyo, ameeleza kuwa walipofika Manyoni abiria walimkataa dereva huyo na kuendesha dereva mwingine wa akiba ambaye naye alikuwa akiendesha kwa mwendo wa kasi kuliko yule wa mwanzo hadi tairi lilipopasuka na kusababisha ajali.

Alisema alipofuatilia kwa karibu aligundua sababu ya mwendo kasi wa mabasi hayo ni madereva hasa wa mabasi ya kutoka Mwanza kugombea mnara yaani anayekuwa wa kwanza kufika anapewa bonasi na matajiri wa mabasi hayo.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Alhajj Juma Killimbah, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga vituo vya afya, zahanati na hospitali lengo likiwa ni kuwasaidia wananchi wanapokuwa wagonjwa na kupata ajali, lakini amesikitishwa na kitendo cha majeruhi wa ajali hiyo kuona wakipoteza maisha licha ya kuwapo huduma za hospitali karibu na eneo la ajali.

"Ajali imetokea mlima Saranda, pale Kintinku pana zahanati, Maweni pana kituo cha afya na Manyoni pana hospitali ya wilaya ni umbali wa kilomita zisizozidi 20 kwa nini hawa majeruhi wasingepelekwa katika maeneo hayo kwa ajili ya kupata huduma ya kwanza ambayo ingesaidia kuzuia damu zisitoke badala yake wakawachukua na kuwapeleka Dodoma umbali wa zaidi ya kilometa 150," alihoji.

Killimbah aliiomba serikali kuhakikisha inaliangalia jambo hilo kwa karibu na kuwa itakuwa haina maana kuwa na zahanati, vituo vya afya, hospitali kila mahali.

Wakati wa maziko hayo simanzi na vilio na watu kuzimia vilitawala huku kila mtu akimzungumzia marehemu Winjuka kwa jinsi alivyokuwa akijitoa kusaidia jamii katika Wilaya ya Iramba na maeneo mengine ya jirani.

Akiongoza ibada ya mazishi, Askofu Noel Lameck wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Singida Kaskazini, alisema umati wa watu uliokuwapo katika ibada hiyo unaonesha jinsi Winjuka alivyokuwa akiishi vizuri na jamii na kanisa na kumuomba kila mtu kujiandaa kwa kutubu na kuokoka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, akitoa salamu za rambirambi aliagiza kila siku kuhakikisha gari lake linakuwa limewekwa mafuta ili kusaidia kusafiri wakati wote hasa kunapokuwapo jambo la dharura.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Innocent Msengi, alisema halmashauri hiyo tangu itokee ajali hiyo na kumpoteza diwani wao, imetoa ushirikiano na kugharamia mambo mbalimbali yaliyokuwa yakihitajika.



Vijana wa Green Guard wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Iramba, mkoani Singida wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Diwani wa Viti Maalum wa chama hicho, Tarafa ya Kinampanda, Winjuka Mkumbo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Halmashauri 29 zanyemelewa na ugonjwa wa usubi

**Na Sabato Kasika**

UGONJWA wa usubi umetajwa kuenea kwa kasi kwenye halmashauri 29, huku ikielezwa kuwa asilimia 7.02 ya watu wapo katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo nchini.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi - Epidemiolojia kutoka Wizara ya Afya, Dk. Azma Simba, kwenye mkutano wa ushauri wa kitaalamu wa kutokomeza ugonjwa huo uliofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Dk. Simba alizitaja halmashauri hizo kuwa ni Madaba, Mbinga, Mbinga, Namtumbo, Nyasa, Songea, Songea na Tunduru mkoani Ruvuma, huku nyingine zikiwa ni Njombe na Ludewa mkoani Njombe.

"Halmashauri nyingine ni Busokelo, Kyela na Rungwe mkoani Mbeya, Mtama na Lindi mkoani Lindi, Ulanga, Mlimba, Ifakara, Malinyi, Kilosa, Mvomero na Gairo mkoani Morogoro," alisema Simba.

Pia zimo Lushoto, Bumbuli, Muheza, Korogwe na Mkinga ambazo ziko Mkoa wa Tanga, Mufindi mkoani Iringa na Ilejea mkoani Songwe.

"Ugonjwa huu huenezwa na nzi wadogo weusi ambao kitaalamu wanaitwa (black flyers), pia huzaliana katika maeneo yenye misitu na maji yanayotiririka kwa kasi," alisema.

Alisema wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya, inafanya mikakati mbalimbali kuwezesha watu kingatiba kwa maeneo mara moja kwa mwaka au mara mbili kwa mwaka.

"Juhudi zilizofanyika hadi sasa kupitia programu maalumu ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ni pamoja na kuainisha maeneo yaliyoathirika kwa ugonjwa huu kwa kufanya utafiti na tathmini," alisema.

Aliwataja baadhi ya wadau wanaoshirikiana nao katika utafiti huo kuwa ni NIMR, MUHAS, CDC, WHO, KCMC na USAID, na kwamba wamepanga kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

"Tunawaomba wananchi waunge mkono juhudi zetu ili tutimize azma ya kutokomeza ugonjwa huu ifikapo mwaka 2030, kwani hili ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha Tanzania inatokomeza magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele (NTDs) ifikapo 2030," alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini, Dk. Alphoncina Nanai, kila baada ya miaka miwili huwa wanatengeneza mipango ya vipaumbele vya serikali vinavyosaidia katika sekta ya afya.

"Kwa kawaida tunapomaliza hapo huwa tunatengeneza vipaumbele vya WHO kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kupambana na magonjwa nchini Tanzania," alisema Dk. Nanai.

Alitaja miongoni mwa maeneo wanayofanyia kazi kuwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya, kutoa misaada katika tiba, kutengeneza miongozo na mikakati kwa kufuata miongozo ya dunia.

"WHO tunashirikiana kwa karibu na Tanzania katika sekta ya afya ikiwamo kufatilia miradi mbalimbali inayoendelea, kwa lengo la kutathmini matokeo maendeleo yake ili kujua kama ni chanya," alisema.

# Wananchi wamkataa M/kiti, Diwani mbele ya DC

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANANCHI wa Kijiji cha Nanganga Kata ya Nanganga Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wamewakataa Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji chao, Msafiri Mohamedi na Diwani wa kata hiyo, Hamisi Ling'welo mbele ya Mkuu wa wilaya hiyo, Claudia Kitta wakiwatuhumu kufanya ubadhirifu wa fedha za mapato ya serikali ya kijiji kwa kuuza maeneo ya kijiji.

Aidha, wananchi hao wamemtaka mwenyekiti huyo kujiuzulu nafasi hiyo kutokana na makosa yanayomkabili na kudai kwa kushirikiana na diwani wa kata hiyo wamekuwa kikwazo cha maendeleo.

Wananchi hao walitoa tuhuma hizo jana kijijini hapo, katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, uliofanyika katika Kijiji cha Nanganga.

Amandusi Renard, mkazi wa kijiji hicho alisema, Mwenyekiti na Diwani wa kata hiyo wamekuwa na tabia ya kula fedha za mapato ya serikali ya kijiji zinazotokana na miradi ya maendeleo ya kijiji chao.

Alisema, pia mwenyekiti huyo wanamtuhumu kuuza baadhi ya maeneo ya ardhi ya kijiji na fedha kujinufaisha mwenyewe pamoja na diwani kunyume cha taratibu na sheria.

Alisema katika kijiji hicho kuna wawekezaji wengi wanaofanya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo uchimbaji wa madini, lakini fedha wanazolipa wawekezaji hao zinapita kwa mwenyekiti huyo na kujinufaisha.

Naye Sadati Muhidini, mkazi wa kijiji hicho, alidai mwenyekiti huyo amekuwa nguli wa kuuza maeneo ya kijiji na anapoulizwa kuhusu mapato kwenye mikutano ya kijiji huwa mkali katika kutoa ufafanuzi.

Kwa upande wake Fadhili Bakari, alidai mwenyekiti na diwani wa kata hiyo wanashirikiana katika kuuza maeneo ya kijiji na fedha kutia mifukoni mwao jambo linalosababisha kijiji kutopata mapato yoyote.

"Mwenyekiti wa serikali ya kijiji na diwani wetu wamekuwa wakiuza maeneo ya kijiji kimya kimya na fedha za wanatia mifukoni mwao sisi hatumtaki tunakuomba mkuu wa wilaya uondoke nao hao hatuwataki kijijini kwetu hapa," alisema Bakari.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Joshua Sanga, alisema ili kumwondoa mwenyekiti wa serikali ya kijiji kuna sheria maalumu sio kwa njia ya kumzomea katika mkutano wa hadhara.

Mkuu wa wilaya, aliwaomba wananchi hao kuwa watulivu na kufuata sheria ya kumwondoa mwenyekiti na kwa sasa wakati wakisubiri utaratibu wa kisheria waendelee kumtambua kwa vile alichaguliwa kisheria.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kulia), akiwa na wanufaika wa programu ya ufadhili wa masomo ya kilimo ijulikano Kilimo Viwanda, Hillary Gilbert (kushoto) na Winnie Mollel, wakifungua milango ikiwa ni ishara ya kuzindua dirisha jipya la maombi ya ufadhili kwa mwaka 2022/2023, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wataka ukatili kijinsia udhibitiwe vyuoni

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa elimu wameiomba serikali kuweka mikakati ya kukabili tatizo la ukatili wa kijinsia katika vyuo vingi vya elimu ya juu.

Walisema hayo katika kongamano la pili la Kimataifa la kujadili ubora wa elimu (IQEC), lililofanyika jijini Dar es Salaam na kushirikisha wadau kutoka nchi 11 ndani na nje ya Afrika.

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Ochola Wayoga, waandaaji wa kongamano hilo, alisema kuna haja kubwa kwa serikali kuchukua hatua ya kukabiliana na tatizo hilo ili kuwasaidia wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo kufikia malengo yao.

Wayoga alisema bado vyuo vingi vinaendelea kukabiliwa na tatizo hilo na kutahadharisha bila kuchukuliwa hatua za haraka za kukabiliana nalo, wanafunzi wengi watakuwa wanashindwa kufikia malengo.

Alisema katika kongamano hilo lililowashirikisha wadau kutoka nchi mbalimbali, pamoja na mambo mengine walijadili masuala yanayoathiri sekta hiyo ya elimu ndani na nje ya Tanzania. Wayoga alisema wadau wa kongamano hilo, walijadili kwa kina hatima ya sekta ya elimu na kuja na suluhisho la kushauri namna ya kusaidia na kuinua sekta hiyo ndani na nje ya nchi.

Pia alisema kongamano hilo lilitoa fursa kwa watunga sera, na wajumbe kutoka Afrika na nje ya bara hilo, watafiti, wasomi na wanafunzi kubadilishana uzoefu na maarifa kuhusu umuhimu wa elimu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi kimataifa.

Alitaja pia miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa kuwa ni pamoja na serikali kutoa kipaumbele kwa kuwekeza katika elimu ya awali kwa watoto, katika eneo la usawa wa kijinsia na kuwawezesha wasichana kufikia malengo yao kielimu.

"Uwekezaji katika elimu ya awali una matokeo makubwa katika jamii, hivyo serikali ina jukumu la kushirikiana na wadau kuhakikisha wanawekeza pia katika eneo hilo bila kusahau elimu ya juu, eneo la walimu pamoja na vitendea kazi," alisema Wayoga.

Mwenyekiti wa Bodi ya TEN/MET, Faraja Nyalandu, alisema elimu bora ni msingi utakaosaidia kubadilisha ulimwengu na ni vyema serikali za nchi hizo zikaendelea kuwekeza zaidi katika eneo hilo.

Mada nyingine zilizojadiliwa katika kongamano hilo ni pamoja na lugha za kujifunzia, matumizi ya teknolojia za kujifunzia, mabadiliko ya kimataifa kuanzia uimarishaji wa mifumo ya elimu na ufadhili, jukumu la asasi za kiraia (CSOs) katika sekta hiyo.

# DAWASA yajenga vituo 30 huduma kwa umma

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), inajenga vituo 30 vya huduma kwa umma ikiwa ni juhudi za kuboresha usafi wa mazingira kwa wakazi wa jiji hilo na Pwani.

Hatua hiyo inatokana na ongezeko la watu wanaofika katika jiji hilo kwa ajili ya shughuli zao za kila siku na vituo hivyo vitajengwa kwenye masoko, stendi za mabasi pamoja na maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi.

Akizungumza kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa Kitengo cha Usafi wa Mazingira nje ya mtandao DAWASA, Mhandisi Charles Makoye, alisema vituo hivyo vinajengwa katika Manispaa za Kinondoni, Temeke, Ilala, Kigamboni na Ubungo.

Alisema, ujenzi wa vituo hivyo ni moja ya vipaumbele vya mamlaka kuboresha usafi wa mazingira katika eneo lake la kihuduma.

Mhandisi Makoye alisema awamu ya kwanza mradi utahusisha ujenzi wa vituo 30 katika manispaa zote za Mkoa wa Dar es Salaam, hususani kwenye sehemu zenye mikusanyiko ya watu kwa lengo la kupambana na magonjwa ya mlipuko pamoja na kuboresha ussafi wa mazingira wa maeneo hayo.

"Mpaka sasa shughuli za ujenzi zinaendelea katika maeneo ya Tundwi Songani, Buyuni soko la samaki, ofisi ya Kata ya Kigamboni, Kibada stendi, Gezaulole stendi, Gezaulole soko la mazao katika Manispaa ya Kigamboni," alisema.

Pia alisema wanajenga vituo kama hivyo kwenye eneo la Mbande Sokoni, TandikaS, soko la Mbagala Rangi 3, soko la Kampochea na soko la Twangoma katika Manispaa ya Temeke.

"Kwa upande wa Manispaa ya Ilala, shughuli za ujenzi zinaendelea maeneo ya Posta ya zamani, Tabata Kimanga stendi, Soko la Kipunguni, Soko la Kigogo Fresh, Soko la Chanika, Zingiziwa na stendi ya Chanika Videte. Coco Beach, Magomeni Garden, Mwananyamala Msolomi, Mwanamboka, Soko la Bunju, Bunju stendi na Mbweni Mpiji kwa Manispaa ya Kinondoni," alieleza Mhandisi Makoye.

Pia alisema wananajenga vituo vya huduma katika soko la Manzese, soko la Shekilango, soko la Mawasiliano, Stendi ya Mloganzila, Stendi ya Mbezi Luis pamoja na Mabibo EPZA yanayopatikana katika Manispaa ya Ubungo.

Mhandisi Makoye alisema mpaka sasa ujenzi wa vituo hivyo unaridhisha huku mradi huo ukitegemewa kukamilika Novemba 2022.

"Mpaka sasa shughuli za ujenzi zinaendelea katika maeneo yote yaliyoainishwa, tunategemea huduma zitaanza kutolewa mwezi Novemba baada ya kukamilika kwa ujenzi," alisema.

Michael Mativila ambaye ni Mwenyekiti wa soko la Shekilango alisema kasi ya ujenzi wa kituo cha huduma kwa umma katika soko hilo kinatoa matumaini kwa wafanyabiashara wa eneo hilo.

Alisema ujenzi wa vituo vya huduma kwa umma ni sehemu ya mradi wa uboreshaji mazingira unaotekelezwa kupitia serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB).

Mradi huo unahusisha ujenzi wa vituo vya huduma kwa umma, mitambo ya kisasa ya kuchakata kinyesitope pamoja na ujenzi wa mifumo rahisi ya kuondosha majitaka majumbani.





Ukurasa 12

Kilichompa Ruto urais dhidi ya Raila Odinga



Ukurasa 13

'Sivutiwi mbio kukimbilia kuandika katiba mpya'

siasa

JUMATANO AGOSTI 24, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

BURIANI MREMA

# Mwenye ubunifu, ushawishi, mvuta umati, uliyebadilisha fikra za Watanzania wengi

**Na Sabato Kasika**

MACHI 3, mwaka 1995, Augustine Mrema anaondoka CCM na kujiunga na Chama cha NCCR- Mageuzi, miezi michache baada ya kuachia ngazi akiwa na dhamana ya Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana.

Kujiengua CCM kulimnyima ubunge wa Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro na hivyo kwenda kuanza maisha mapya ya kisiasa ndani ya upinzani akiwa na msururu wa wanasiasa aliohama nao kutoka CCM.

Miongoni mwao ni mtu wake wa karibu Thomas Ngawaiya, ambaye alichaguliwa kuwa mbunge wa Moshi Vijijini kuchukua nafasi ya Mrema aliyewania urais katika uchaguzi wa mwaka 1995 kupitia NCCR- Mageuzi.

Nipashe inazungumza na Ngawaiya anayemwelezea Mrema kuwa alikuwa kiongozi mbunifu na mwenye ushawishi mkubwa katika siasa za Tanzania aliyeungwa mkono na watu wengi.

Aidha, alikuwa na kipawa cha kuvutia umati (crowd puller), ambaye aliposimama kusanyiko kubwa lilimfuata kumsikiliza.

"Nilikuwa mmojawapo wa watu waliohamia NCCR-Mageuzi kumfuata Mrema, kutokana na utendaji wake uliotukuka alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa awamu ya pili," anasema Ngawaiya.

Aidha, anasema, waliozaliwa miaka ya 90 hawawezi kujua mambo makubwa ambayo Mrema aliifanyia nchi ikiwamo kuamuru majambazi kujisalimisha na kukabidhi silaha polisi na walifanya hivyo.

Kadhalika alipambana na rushwa na dawa za kulevya bila woga na alifanikiwa 'kuteka' mioyo ya Watanzania kutokana na utendaji kazi bila kujali cheo cha mtu wakiwamo vigogo waliokuwa wakijihusisha na rushwa na masuala haramu.

"Mrema aliwahi kumnasa mkubwa mmoja katika uwanja wa ndege jijini Dar es Salaam, akisafirisha dhahabu, ndipo lilipoanzia jina la kigogo, kwani yeye alisema amemkamata kigogo aliyekuwa na nafasi kubwa serikalini," anasema.



Mrema (kushoto) enzi hizo akiwa na swahiba wake Thomas Ngawaiya kwenye viwanja vya bunge jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

## VITUO MITAANI

Mwanasiasa huyo aliyeaga dunia Jumapili iliyopita, wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kipindi hicho, vituo vidogo vya polisi vilijengwa kwa wingi nchini, ili kusogeza huduma za jeshi hilo karibu na wananchi mijini na vijijini.

Wananchi walitoa ardhi kujenga vituo hivyo bila kudai fidia wala kulalamikia utekelezaji wa maagizo hayo.

"Hatua hiyo ilikwenda sambamba na uimarishaji wa sungusungu, lakini hata usiku wa manane Mrema alikuwa anaweza kuamka na kuzunguka baadhi ya maeneo kuangalia hali ya ulinzi," anasema.

Ngawaiya anaongeza kuwa Mrema alikuwa na uwezo na ujasiri wa kuwaamuru majambazi ndani ya siku saba kujisalimisha na silaha zao polisi na wahusika wakatekeleza agizo hilo.

Juhudi za kupambana na rushwa kwa nguvu zake zote hadi akapachikwa jina la Sokoine, zilionekana.

Anasema hayo yote yalikuwa yanaonyesha ni jinsi gani alivyokuwa akifanya kazi yake, ili kuhakikisha raia na mali zao wanakuwa salama na kwamba kwa juhudi hizo Watanzania wanyonge walimpenda.

"Wanyonge hao ndiyo ninaamini kuwa hata alipohama kwenda upinzani walijitokeza kwa wingi kumfuata huko, nikiwamo mimi, kwani tulishaona utendaji kazi wake, kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania," anasema.

## KUHESHIMU KAZI

Anakumbushia kuwa Mrema alitaka watu wachape kazi, kila mmoja ale kwa jasho lake na alifikia kuelekeza wafanyakazi kuwahi kazini anayechelewa kiti chake kiondolewa, na kweli wafanyakazi walipunguza uchelewaji ofisini.

Ngawaiya anaongeza kuwa katika utendaji kazi huo, alichukiwa na baadhi ya wafanyakazi na viongozi wa umma waliodai kuwa anavuka mipaka.

Hili halikumkatisha tamaa Mrema aliendelea kuwabana zaidi, anaongeza.

"Utendaji wake ulivuta wengi ndani ya CCM na nje ya chama kwa kuungwa mkono na kada mbalimbali wakiwamo wasomi na wataalamu wengi, lakini alipobadilishwa wizara tuliona kuwa kile alichokusudia kukifanya kwa ajili ya Watanzania hakiwezi kutimia," anaongeza.

Anasema hata Mrema mwenyewe aliliona hilo akaamua kujiondoa mapema CCM na kuhamia upinzani ili kuendeleza harakati zake za kuwatumikia wananchi akiwa nje ya chama hicho tawala.

Mwanasiasa huyo anasema Machi 3 mwaka 1995, ni tarehe rasmi ambayo Mrema na wafuasi wake walijiunga NCCR- Mageuzi na kuleta hamasa kubwa katika siasa, akateuliwa kuwa mwenyekiti wa chama hicho na baadaye mgombea urais.

Ngawaiya ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA), anasema chama hicho kilimpitisha Mrema kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa 1995.

"Katika uchaguzi huo, Mrema alileta upinzani mkali kwa mgombea urais kupitia CCM Benjamin Mkapa (sasa ni marehemu) uliomshtua Baba wa Taifa Julius Nyerere, hadi kujitokeza kumpigia debe baada ya kuona nguvu na moto wa kampeni za NCCR-Mageuzi zikimkandamiza mgombea wa CCM," anasema.

Anafafanua kuwa kujitokeza

INAENDELEA UK. 14

# Kilichompa Ruto urais dhidi ya mkongwe Raila Odinga

- Raila adaiwa mradi wa rais usio na jipya
- Ruto apokelewa shujaa wa mawazo mbadala



William Ruto, Rais Mteule wa Kenya anayevaa tabasamu muda wote licha ya mpinzani wake kutinga kortini. **PICHA MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WILLIAM Ruto, Jumatatu iliyopita Agosti 15, Tume ya Uchaguzi ya Kenya inamtangaza kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais akipewa cheti cha kuiongoza serikali ya awamu ya tano.

Kwa tangazo hilo, kilichojiri ni kwamba Naibu Rais Ruto alikuwa amewapiga bao la kisigino wakubwa zake wake wawili wa zamani na washirika wake kwenye siasa za vyama vingi, 'mgombea wa kudumu' kila uchaguzi wa urais Raila Odinga na mtetezi wake au swahiba wake Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Ruto anajitangaza kuwa mpambanaji aliyeuza kuku na karanga mitaani, anayeahidi kutoa suluhisho bora la kiuchumi kuliko enzi za Odinga na Kenyatta walivyofanya au wangepanga kufanya.

Katika kampeni, rais mteule Ruto alikwepa kwa ustadi kuzungumzia masuala ya ukabila ambayo yamekuwa msingi mkuu wa siasa na uongozi unaoitawala Kenya.

Badala yake, aliyataja masuala ya ukabila au kuyahusisha na vita vya kitabaka kati ya walio nacho (mtajiri) wanaotokana na siasa na wasio nacho au Wakenya wengi maskini wasio na kitu.

Ni kutokana na mawazo yake alijifanya mnyenyekevu tofauti na wapinzani wake ambao kisiasa wana 'nasaba' , damu ya kundi la wenye nacho au matajiri wa kisiasa ni kifedha wa taifa hilo.

> Kwa kufanya hivyo, alihamasisha ukosefu wa usawa na pengo kati ya matajiri na maskini na kudhoofisha uhamasishaji wa siasa kwa misingi ya kikabila.

"Kwa kufanya hivyo, alihamasisha ukosefu wa usawa na pengo kati ya matajiri na maskini na kudhoofisha uhamasishaji wa siasa kwa misingi ya kikabila," unasema mtandao wa Al Jazeera.

Maridhiano au 'handshake' kati ya Odinga na Kenyatta, ni tukio kubwa ambalo linajulikana katika siasa za Kenya kama "kushikana mikono" ndilo lilimtimua Ruto kwenye kurithishwa uongozi na Kenyatta.

Naibu Rais huyo akiondolewa kuwa mgombea wa nafasi hiyo baada ya muhula wake wa pili wa miaka mitano, akiwa chini ya Kenyatta.

Katika kampeni yake, kambi ya Ruto ilishikilia madai kuwa Kenyatta alikengeuka kutoka kwenye ajenda ya utawala waliyokubaliana wawili hao, Ruto akionekana kama amesalitiwa, hivyo kupata kura za huruma kutoka kwa Wakenya.

Deni la taifa limeongezeka mno kwenye utawala wa Kenyatta, kutoka Shilingi trilioni 1.89 za Kenya (Dola bilioni 21.95 mwaka 2013 hadi kufikia Shilingi trilioni 8.59 (Dola bilioni 71.85) sasa ikionyesha kuwa serikali yake iliitegemea mno mikopo kwa ajili ya miradi ya miundombinu inayohitajika sana.

Lakini uongozi wao unachafuliwa na ukosefu wa ajira uliokithiri, jambo linalosababisha malalamiko na kufadhaika miongoni mwa Wakenya hasa vijana ambao ni theluthi mbili ya raia wengi wakiwa chini ya miaka 35.

Aidha, janga la COVID-19 na uvamizi wa Russia nchini Ukraine ulifanyika baada ya kitisho la UVIKO-19 umeongeza matatizo kwenye uzalishaji na usambazaji wa chakula na kupandisha kupindukia gharama za maisha nchini humo kama ilivyo mataifa.

Kwa hivyo Ruto alitumia hali hizo kuwa mtaji wa kisiasa kuwashawishi Wakenya wampigie kura ili kulinda 'matumbo yao' na si vinginevyo "Alijitambulisha na kujifananisha na wanaokwenda kwenye 'supamaketi' lakini hawana pesa za kununua kile wanachokiangalia," inaongeza Al Jazeera.

"Raila Odinga ulikuwa mradi wa Rais Kenyatta ambaye serikali yake aliharibu uchumi wetu," "Ruto alikuja na mpango wa kiuchumi ambao ulilenga kuleta mabadiliko katika maisha ya raia wengi. Watu waliona mpango huo kama njia ya ustawi wa kiuchumi na si vinginevyo."

Lakini, huku Ruto kwenye kampeni zake anasisitiza kupanda kwa gharama za maisha kunawaumiza raia, lakini ukabila ulikuwa bado ukinyemelea kila mara, kwa kuwa naye ni nasaba ya makabila makuu yaliyotawala Kenya.

**RUTO MABONDE/MILIMA**

Baada ya kurudishwa siasa za vyama vingi mwaka 1991, chama tawala cha KANU kilianzisha mrengo wa vijana ili kuwachombeza wapigakura vijana kabla ya uchaguzi mwaka uliofuata wa 1992. Lengo lilikuwa kuwezesha muhula wa nne wa Rais Daniel Moi ( sasa ni marehemu )madarakani.

Iliitwa Youth for Kanu (YK92) na ndicho kilichomleta Ruto, mmoja wa viongozi wake, kwenye anga za kitaifa na kumfahamisha kwa Wakenya.

Ilipofika 1997 akiwa na miaka 31 mbinu zake za kisiasa zilikuwa madhubuti na za hali ya juu akimshinda mbunge wa muda mrefu wa Eldoret Kaskazini, mkongwe Reuben Chesire na kutwaa ubunge wa jimbo hilo.

Ruto mwenye digrii za botani, zoolojia na shahada ya juu (PhD) ya ikolojia ya mimea baadaye ameshika majukumu mbalimbali serikalini kuanzia bungeni hadi baraza la mawaziri.

Alijionyesha zaidi kuwa mwanasiasa mwenye azma, baada ya kumuunga mkono Kenyatta ili awe rais mwaka wa 2002, akijiondoa kwenye kugombea, lakini miaka mitano baadaye ili kumuunga mkono mtiania Odinga kuwa rais alijiengua pia kwenye kugombea urais.

Mwaka 2013, Ruto aliwania wadhifa wa urais pamoja na Kenyatta lakini ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007 ambazo zilisababisha vifo vya watu 1,500 na wengine zaidi ya 500,000 kuyahama makazi yao, akawa gumzo kubwa nchini mwake.

Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) iliwashukia wawili hao kwa uhalifu dhidi ya ubinadamu kwa madai ya kuhusika na kuchochea ghasia katika kipindi hicho, walikuwa wamechaguliwa kuongoza Kenya lakini waliondolewa kinga kuhudhuria kesi hiyo nchini Uholanzi lakini walifutiwa mashtaka kutokana na ushahidi dhaifu.

Baada ya kuachiwa, Ruto, ambaye mara kwa mara anatembelea na kutoa michango makanisani alisema anamwamini "Mungu wake wa haki na ushindi" kumtetea.

Wakati wa kesi ya Kenyatta mwaka 2014, Ruto alishika nafasi ya urais kwa siku tatu. Muda huo mfupi kama kiongozi wa taifa uliimuimarisha kiimani na kumchochea kuwa rais kamili.

Huku Kenyatta akimtosa kwenye shughuli za serikali baada ya "kupeana mkono", Ruto alitafuta wadau wapya wakiwamo wanasiasa waliotengwa na muungano wa Jubilee Party, inasema Al Jazeera.

Muda si muda kulikuwa na makundi mawili serikalini, moja likimuunga mkono Kenyatta na lingine Ruto.

Vuguvugu lake la wafuasi wengi nchini Kenya Kenya Kwanza' lililenga sio tu ngome zake bali pia vijana wasio na kazi na maeneo ya upinzani.

Cha kufurahisha rais mteule amepata ushindi nyumbani kwa Kenyatta na kwa mgombea mwenza wa Odinga Martha Karua.

ALI AMEIR MUHAMMED

# ‘Sivutiwi mbio kukimbilia kuandika katiba mpya’

## • Anasimamia viraka kila yanapotajwa mabadiliko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

“KATIBA sio Msahafu inahitaji kufanyiwa marekebisho lakini sio kuiondoa kabisa iliyopo. Kinachohitajika ni kubadilisha maeneo kadhaa kwenye hii iliyopo ili kuwa na nyingine inayokwenda na wakati.”

Ni msimamo wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Ali Ameir Muhammed, aliyehudumu wakati wa Rais Benjamin Mkapa, aliyeongoza awamu ya tatu, anapozungumza na Nipashe nyumbani kwake Kijiji cha Donge mjini Zanzibar.

Anaeleza hakuna haja ya taifa kugharamika kuwa na katiba mpya bali iliyopo irekebishwe vipengele ambavyo havipo sawa kuepusha kuingia gharama kubwa ya kuandika nyingine, badala ya kufanyakazi za maendeleo ya wananchi.

“Msimamo wangu katiba inahitaji kubadilishwa kila wakati lakini si kugharamika kuandika mpya,” anasema na kuongeza kuwa Watanzania wanaelewa kuwa ni raia wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Zanzibar na Tanzania Bara na wanafahamu Zanzibar ina haki gani katika muungano huo.

Anasema kulikuwa na machafuko ya kuushambulia muungano hivyo uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, utaondoa malalamiko hayo.

Ameir anakoshwa na uongozi wa Rais Samia kwa sababu anaimudu kazi yake ambayo inahusu kuongoza makabila ya watu mbalimbali na yanayokubali kuwa kiongozi ni mwanamke.

“Namvulia kofia Rais Samia anaimudu kazi yake nimeishi sana Bara kuna baadhi ya makabila ni magumu hivyo kukubali kuwa nchi inaongozwa na rais mwanamke ni mafaniko makubwa kitaifa,” anaongeza mwanasiasa huyo mkongwe.

**KUONDOA MALALAMIKO**

Anasifu Tanzania kuongozwa na Rais Samia, akisema kumepunguza malalamiko ya kuwa Zanzibar inaonewa katika masuala ya Muungano wa Tanzania hivyo ni jambo la kujivunia.

Anawataka Watanzania kuendelea kushirikiana na kumuunga mkono Rais Samia ili nchi iendelee kujipatia maendeleo kwa kushirikiana na viongozi wengine wa serikali zote mbili akiwamo Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar.

Kwa upande wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ameir anampongeza kwa kazi kubwa ya kuwaunganisha wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba katika serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Anasema Zanzibar inakabiliwa na siasa zenye ushindani tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi ambazo zimekuwa na changamoto nyingi na njia pekee ni kutekeleza maridhiano ya kisiasa kwa ajili ya kuwaunganisha Wazanzibari.

“Nachukua nafasi hii kumpongeza Rais Mwinyi ameanza vizuri katika kutekeleza maridhiano ya kisiasa na amefaulu. Tunashuhudia utulivu wa kisiasa ukizidi kuimarika huku maendeleo ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa shule na hospitali ukitekelezwa Unguja na Pemba,” anaongeza.



Ali Ameir Muhammed. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

> “Kumepunguza malalamiko ya kuwa Zanzibar inaonewa katika masuala ya Muungano wa Tanzania hivyo ni jambo la kujivunia.



Rais Hussein Ali Mwinyi

Anamsifia Mwinyi kuwa amefanya kazi kwa karibu na viongozi wanne wa taifa, kuanzia Rais Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete kwa upande wa Bara na Dk. Salmin Amour Zanzibar hivyo ameshiba kiuzoefu na kiuongozi.

Anakumbusha kuwa wakati wa awamu ya Mkapa alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, lakini alikuwa bosi wake kabla ya kuwa rais wakati akiwa Mhariri Mkuu wa magazeti ya Uhuru na Mzalendo.

Waziri huyu mstaafu aliyewahi kuwa mbunge wa jimbo la Donge kwa muda wa miaka 10 bila ya kuwa na mpinzani, anaitaja siri ya mafanikio yake ni kuwa kiongozi imara kwa kuwaongoza wananchi ambapo udhibiti wa kisiasa na kiitikadi ulikuwa imara.

**MAFANIKIO KIUONGOZI**

Akieleza kuhusu mafanikio yake wakati akiwa waziri, Ali Ameir, anasema alishika nafasi hiyo kwa muda wa miaka minne na anashukuru kuwa alitumikia dhamana hiyo bila ya kutumbuliwa na anaamini kuwa alitimiza wajibu wake wa kumsaidia rais ipasavyo.

“Sipendi kujivisha kilemba cha ukoka. Lakini wakubwa wangu walioniteua waliona kuwa kuna kazi inafanyika na hata Rais Mkapa alipofanya mabadiliko sikuwa nje ya Baraza la Mawaziri nilipewa wizara inayohusiana na masuala ya habari,” anasema.

**AWAGEUKIA VIJANA**

Ameir anawashauri vijana wasiwe na haraka wala tamaa ya kutamani maendeleo kwa haraka bali wafanye jitihada ya kuchapa kazi, kupata elimu na kujua namna ya kumudu maisha yao kwa riziki halali, lakini pia kutambua na kuheshimu viongozi wanaowaongoza.

“Vijana lazima wapende maendeleo lakini katika kutamani wasiwe na haraka sana. Maana kuna wakati tulikuwa tunapambana na watukutu sana lakini nashukuru tulikaa nao na tukawalea na kwa sasa wamebadilika,” anasema bila kufafanua.

Hakumsahau swahiba wake mkubwa kisiasa, mstaafu wa Zanzibar Dk. Salmin Amour, wakati yeye akiwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM -Zanzibar, ambaye anakiri alifanya kazi naye kwa karibu kwenye mazingira ya wakati huo ya mfumo wa vyama vingi.

“Kulikuwa ndiyo kwanza mfumo unaingia ukiwa na joto kubwa la vuguvugu la kisiasa. Kwa mfano itakumbukwa katika kipindi cha pili cha uongozi wa wa Salmin Amour, ndiyo mageuzi ya kisiasa na kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi. Ndiyo wakati CCM ilipambana na Chama cha Wananchi -CUF kilichokuwa kikiongozwa na Maalim Seif Sharif Hamad (marehemu).”

Anamsifu Dk. Salmin kwa uhodari na kwamba hakuwa akiendesha nchi kwa mabavu kama wanavyodai baadhi ya watu bali aliwajibika kwa Wazanzibar.

“Nauhusudu uongozi wa Dk. Salmin alikuwa ni kiongozi imara anayejiamini na nimefanya naye kazi kwa karibu kuliko marais wote,” anasema na kuongeza.

# Mwenye ubunifu, ushawishi, mvuta umati, uliyebadilisha fikra za Watanzania wengi



Mwili wa Mrema utaagwa leo nyumbani kwake Salasala Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK. 11**

kwa Baba wa Taifa kumsimamia mgombea wa CCM, kulimpa Mkapa ushindi huku NCCR-Mageuzi ikijizolea viti 17 vya ubunge katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

**KUVUNJA NGOME**

"Wakati huo tulishinda ubunge katika mikoa ngome yenye wasomi, wafanyabiashara, watu wenye uelewa wa siasa na mwelekeo wa uchumi duniani.

Ni Dar es Salaam katika Jimbo la Ubungo, Arusha Mjini, Muleba Kaskazini mkoani Kagera, Mbeya Mjini, Iringa Mjini, Moshi Vijijini na Hai mkoani Kilimanjaro," anakumbusha.

Akieleza kuwa kupata ushindi kwenye miji mikubwa na mikuu kama Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na Iringa na si vijijini ilionyesha jinsi Mrema alivyoleta mabadiliko ya kifikra, kueleweka na wapigakura kuamua kukubalika.


Anataja majimbo mengine kuwa ni Musoma Vijijini, Mwibara, Rorya na mkoani Mara, Vunjo mkoani Kilimanjaro na Urambo mkoani Tabora, huku akichaguliwa kuwa mbunge wa Moshi Vijijini.

"Ukweli ni kwamba, Mrema alikuwa ni chachu kubwa ya mageuzi ya siasa za vyama vingi nchini, alifungua njia ya upinzani kuwa na wabunge na madiwani wengi baada ya kurejeshwa mfumo vyama vingi," anakumbusha.

Mwanasiasa huyo anasema, uswahiba kwa Mrema ulifikia hatua ya kutoa ghorofa yake iliyopo Manzese Argentina kuwa makao makuu ya chama hicho, lakini baadaye mwaka 2005 akaamua kurudi CCM.

"Katika maisha, kutofautiana kimawazo na kimtazamo ni jambo la kawaida, hivyo na mimi tulitofautiana nikaamua kurudi CCM, lakini ninatambua mchango wake katika mageuzi ya Tanzania," anasema.

> "Ukweli ni kwamba, Mrema alikuwa ni chachu kubwa ya mageuzi ya siasa za vyama vingi nchini, alifungua njia ya upinzani kuwa na wabunge na madiwani wengi baada ya kurejeshwa mfumo vyama vingi.



Mrema na mkewe Rose enzi za ujana wao.

**UJASIRI, KUJIAMINI**

Kumbukumbu wakati wa kampeni zinaonyesha kuwa Mrema bila woga, aliwatuhumu viongozi wakuu serikalini akiwahusisha na rushwa kutoka kwa wawekezaji.

Wakati wa kampeni ya uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Temeke Dar es Salaam mwaka 1996, alilipua mabomu kadhaa akiwashambulia.

Aidha, alilipua bomu la kashfa ya mlungula wa minofu ya samaki ndani ya Wizara ya Fedha na kusababisha viongozi kuachia ngazi.

Madai yake yaliundiwa Kamati ya Bunge kuchunguza nyaraka zilizokuwa zikihusisha tuhuma za rushwa dhidi ya vigogo mbalimbali wa serikali ya CCM.

Sakata halikuishia hapo, alifikishwa mbele ya kamati hiyo ili kutoa ushahidi, lakini aliona kuwa kitendo hicho kililenga kumwondolea imani kwa jamii ili kuonekana kama mhuni.

Mrema anakumbukwa na mengi aliyoyafanya akiwa waziri na hata alipohamia upinzani wakati akiwa na nguvu kubwa za kisiasa, yanaonyesha ujasiri na ushujaa bila woga.

**MBUYU UMENG'OKA**

Hamad Tao ni mmoja wa watu wa karibu na Mrema, aliyejitoa kwa kila hali ili kuhakikisha mwanasiasa huyo anaendelea kuongoza mageuzi nchini, anapozungumzia kifo cha mwanasiasa huyo, anasema mbuyu umeng'oka.

"Mrema alikuwa kiongozi imara ingawa kama walivyo binadamu wengine alikuwa na udhaifu ila alisaidia kuimarisha mageuzi nchini kutokana na utendaji wake uliotukuka na kuaminiwa na Watanzania," anasema Tao na kuongeza kuwa hakuwa tayari kuyumbishwa kwa maslahi binafsi badala yake alisimamia kuhakikisha upinzani unakuwa imara na kwamba kilichomyumbisha ni uvamizi wa mamluki katika upinzani.

"Uvamizi wa mamluki ulisababisha hadi mimi na Mrema kutofautiana, tukiwa TLP wakati huo nikiwa Naibu Katibu Mkuu wa chama, lakini ukweli ni kwamba alikuwa kiongozi madhubuti," anasema.

Tao anasema wapo wengi ambao hawakupenda kuona upinzani unaimarika na kusababisha mvurugano, kwa lengo la kutaka kuonyesha umma kuwa Mrema hafai na kwamba wahusika walifanikiwa katika hilo.

Lakini pamoja na hayo, ni kwamba Tanzania imepoteza mtu muhimu katika siasa ingawa kwa muda mrefu alikuwa na tatizo la kiafya lililosababisha ashindwe kufanya siasa kikamilifu," anasema.

**MWINYI, MKAPA WAMTAJA**

Marais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi na Mkapa awamu ya tatu katika vitabu vyao, wanakiri kuwa Mrema aliwapa 'kashkash' katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995.

Katika kitabu cha 'Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anaelezea kwa kina alivyomtumia Mrema akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuwashughulikia viongozi walioandamana bila kufuata sheria, akiwamo mwanasheria Mabere Marando mwanzoni mwa miaka 1990.

Katika ukurasa wa 269 wa kitabu chake, Mwinyi anasema baada ya kuanzisha upinzani nchini, hakuwa na wasiwasi na hiyo ilikuwa kabla Mrema hajahamia upinzani, lakini mambo yalibadilika kutokana na uamuzi wake huo anaokiri uliwasumbua na 'kuwachangamsha kidogo'.

Kwa upande wake Mkapa, ndani ya andiko lake la 'My Life My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu)' ukurasa wa 109 hadi 110, anaeleza jinsi uchaguzi wa mwaka 1995 ulivyokuwa mgumu na walivyofanikiwa kumshinda Mrema.

Anabainisha kuwa Mrema aliwasumbua kutokana na uamuzi wa haraka usiokuwa na busara, kwamba aliwahi kuwa kiongozi mwandamizi serikalini, hivyo alijua kazi za serikali na aliwahi kwa wananchi kama namna ya kujikinga, akiwa makali kwa jamii ya watu wenye asili ya India ambao walikamatwa hata kama hakuwa na madaraka hayo.

"Jamii ilimwona kama mtu imara anayeweza kuipeleka nchi mbele kutokana na kusambaa taarifa kuwa serikali ya CCM haikuwa inafanya vizuri, chama kiliogopa huenda wananchi wangemchagua Mrema.

"Baadhi ya watu walisema hatumjui Mkapa, tunajua alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na hajui siasa," Mkapa anasimulia katika kitabu chake hicho.

Mrema alifariki dunia Jumapili iliyopita katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alikokuwa anapatiwa matibabu na atarajiwa kuzikwa kesho kijijini kwake Kiraracha mkoani Kilimanjaro.



# Apigia debe kilimo mkonge

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mkonge Tanzania, Mariam Nkumbi, amewataka wananchi hasa vijana kujikita kwenye kilimo cha zao hilo ili wajikwamue kiuchumi.

Akizungumza na gazeti hili juzi, mwenyekiti huyo alisema, mkonge ni zao ambalo linavunwa kwa muda miaka 15 na kwamba linarahisisha mtu kujikwamua kiuchumi pamoja na familia yake.

Zao hilo, alisema hivi sasa lina soko kubwa nchini na nje ya nchi, hivyo ni vyema wakulima wakachangamkia fursa ya kilimo hicho ili kujikwamua kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa serikali imewekeza kwenye kilimo.

Alifafanua kuwa uwekezaji wa mkonge ni mzuri kwa kuwa mtu akishaupanda kuvuna ni kwa muda wa miaka 15 mfululizo.

Kutokana na hilo ameihamasisha jamii ijikite kwenye kilimo cha mkonge kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Pia aliwaasa vijana kuacha kuzurura bila kazi na badala yake wajikite kwenye shughuli mbalimbali ikiwamo katika kilimo cha mkonge ambacho kitawapatia kipato cha kujikimu wao na familia zao.

"Mkonge ni njia pekee ya kuwawezesha na kuwainua wananchi hususan vijana kiuchumi, ukipata eneo lako la zao mkonge ukaweka katika kipindi cha miaka 15 wewe utakuwa unavuna tu," alisisitiza.

Vile vile alisema, kujikita katika zao hilo la mkonge na kumwezesha muhusika kupata mikopo ya riba nafuu kutoka benki itakayowawezesha kulima kwa tija.

"Nawakaribisha mpite kwenye ofisi zetu mpate maelezo namna ya kufanya katika kilima zao hilo na sasa hivi benki nyingi zinatoa mikopo ambapo mkonge ni zao mojawawapo ambalo benki inaliangalia katika kutoa mikopo kwa vijana hasa kwenye kilimo ambayo imeshushwa riba," alisema.

# Ofisi za Magereza na Uhamiaji zanusurika kuteketea kwa moto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma limenusuru jengo la ofisi za Magereza na Jeshi la Uhamiaji kuteketea baada ya kuzuka moto mkali katika karakana iliyo jirani na majengo hayo.

Tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 1:15 asubuhi katika karakana hiyo ya kutengeneza samani mbalimbali za mbao zikiwamo makochi, viti, meza, milango na madirisha.

Akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la tukio Kamanda wa Operesheni wa Zimamoto na Ukokoaji Mkoa wa Dodoma, Deogratius Inano, alisema wamefanikiwa kuudhibiti moto na kuufanya usisambae katika maeneo mengine ya jirani.

"Tulikiwa ofisini tuliona wingu zito la moshi katika maeneo haya tukaja bila kupewa taarifa na wahusika tukakuta moto ni mkali sana kutokana na karakana hii kuwa na vitu vingi ndani yake ambavyo ni chakula cha moto.

"Tumekuta moto unasambaa kwa kasi sana kwani humu ndani palikuwapo na bidhaa za mbao kama makochi, milango, meza na vumbi la mbao ambalo lilikuwa linaongeza sana moto," alisema Inano.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamelazimika kutumia zaidi ya saa tatu kuuzima moto huo ambao ulikuwa unakaribia kuingia katika majengo mawili ya ofisi za Jeshi la Magereza na Uhamiaji ambayo yako jirani na karakana hiyo.

"Tunashukuru Mungu moto huu haujaathiri mtu hata mmoja hadi sasa lakini mali zilizokuwapo zote zimeteketea katika karakana na nyumba moja ya jirani yenye vyumba vitatu kimoja ndicho kimeteketea," alisema.

Aidha, alisema chanzo cha moto huo bado hakijafahamika na jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola vinaendelea na uchunguzi.

"Kuna watu ambao walikuwapo eneo hili wakati moto huu unaanza. Tumewachukua kwenda kuwahoji ili kubaini nini sababu ya moto huu lakini pia na sisi tunaendelea na uchunguzi wetu kutafuta sababu ya moto huu," alisema.

Kadhalika, aliwataka wakazi wa mkoa wa Dodoma pamoja na wafanyabiashara kuweka vifaa vya kuzimia moto katika maeneo yao ili kusaidia pindi linapotokea janga kama hilo.

"Lakini karakana hii haipaswi kuwapo katika maeneo ya makazi inapaswa kuwekwa nje ya mji, hivyo nitoe rai kwa wananchi kwenda kwenye mamlaka husika ili kupatiwa maeneo sahihi kwa ajili ya viwanda kama hivi.

"Lakini linapotokea janga kama hili watu watupigie simu kupitia namba yetu ya bure kwani hapa tumekuja lakini hatukupigiwa hata simu na wahusika," alisisitiza Inano.

Mmiliki wa moja ya nyumba zilizoungua, Karim Bhanji, alilishukuru jeshi hilo kwa kazi nzuri walioifanya ya kusaidia moto huo usisambae na kuteketeza vitu vingi.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakizima moto ulioteketeza karakana ya kutengeneza samani katika Barabara ya Sita, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yavalia njuga watoto wa mitaani

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imejipanga kushirikiana na wadau mbalimbali kupunguza idadi ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Akizungumza katika kikao na Taasisi ya Azaria Foundation jijini hapo juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, aliitaka jamii kuwa na upendo katika familia na kuhakikisha watoto wanatunzwa ili wapate malezi na makuzi bora.

"Familia inaposhindwa kwa namna yoyote ile, sisi jamii tuchukue wajibu na tuungane na wadau hawa kutatua shida hii. Wizara tumejipanga kwa kushirikiana na wadau kutumia mbinu zote," alisema Dk. Chaula.

Naye Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Azaria Foundation, Audax Abeli, ambaye ameishi maisha ya mtaani, alisema familia yake ilikuwa chanzo cha yeye kuitwa mtoto wa mtaani jina ambalo si sahihi.

"Hili tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani linatakiwa kushughulikiwa kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa. Tunaweza tukapunguza watoto wa mtaani. Pia changamoto nyingine zinatokana na familia," alisema Audax.

Alieleza kuwa mpaka sasa taasisi hiyo inahudumia watoto 70 kwa kuwapatia huduma muhimu za kijamii na mbinu mbadala za kupambana na maisha.

Kamishna wa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Nandera Mhando, alisema wizara itashirikiana vyema na mdau wa taasisi hiyo kwa kusaidiana na timu ya wataalamu inayofanya kazi ya kushughulikia watoto wanaoishi mazingira magumu na kuwatoa mtaani.

"Moja ya miradi itakayozinduliwa hivi karibuni ni wa ujenzi wa kituo cha kupokea watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na kuwapitisha katika mabadiliko ya tabia na ujuzi ili wanaporudi majumbani wajiajiri," alisema Dk. Mhando.



# Makarani sensa mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKATI Sensa ya Watu na Makazi ikiwa imeanza nchi nzima, makarani wawili wametiwa mbaroni wakichunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mbeya kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa kwenye mchakato huo.

Makarani hao wamekamatwa na TAKUKURU kwa tuhuma za kupokea fedha taslimu Sh. 400,000 kutoka kwa watu wawili tofauti ili wawapatie ajira ya kushiriki kwenye sensa mkoani hapo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Hawa Kajula ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sinde jijini Mbeya na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlimani ya jijini Mbeya, Baita Sanga.

"Maeneo yaliyoonekana kuwa na dosari katika sensa ya watu na makazi ni kwenye mchakato wa kuwapata makarani. Tumebaini kuwa mchakato huo kwenye ngazi za kata kulikuwa na upendeleo na vitendo vya rushwa vimetumika kuwapata badala ya vigezo vilivyowekwa," alisema Ndimbo.

Alisema baada ya TAKUKURU kutilia shaka mchakato huo, iliweka mtego ambao ulifanikisha kuwanasa watumishi hao wa umma na ndipo uchunguzi wa kina ukaanza ili kupata ushahidi na hatimaye kuchukuliwa hatua.

"Taarifa tulizozipata ni kwamba watuhumiwa hao kila mmoja alipokea Sh. 200,000 kutoka kwa vijana waliokuwa wakitafuta ajira ya kuhesabu watu na sasa tunaendelea kulifanyia kazi suala hili," alisema Ndimbo.

Alisema kwa sasa wasimamizi hao tayari wameondolewa kwenye usimamizi wa mchakato huo wa sensa na hatua za awali za uchunguzi wa suala hilo zimeashaanza kuchukuliwa.

Ndimbo alisema kwa watahiniwa ambao walipendelewa kwenye usahili wa sensa, walinyimwa sifa za kuchaguliwa na wale ambao walipunjwa maksi walipewa sifa za kuchaguliwa kuwa makarani wa sensa.

Aliongeza kuwa hadi sasa bado wanaendelea na uchunguzi ikiwa ni pamoja na kushikilia simu zao ili kubaini miamala iliyoingia kufahamu fedha zilizoingia na ikithibitika watafikishwa mahakamani.

Ndimbo alitoa rai kwa wadau wote wa sensa kujiepusha na vitendo vya rushwa na udanganyifu au kutumia nafasi ya usimamizi wa sensa kufanya uovu na kwamba wananchi kuwa makini.

Aliwakumbusha makarani kutekeleza majukumu ya kuhesabu watu kwa uaminifu lakini kutunza vitendea kazi hadi zoezi litakapokamilika.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), akijibu maswali kutoka kwa karani wa Sensa ya Watu na Makazi nyumbani kwake, Iwambi, jijini Mbeya jana. PICHA: GRACE MWAKALINGA

## Mil. 507/- kumaliza uhaba maji Chunya

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imetoa Sh. milioni 507 kwa ajili ya kukamilisha mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Sangambi, Chunya mkoani Mbeya.

Mradi huo unatajwa kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji katika eneo hilo na kuhudumia maeneo yanayozunguka kata hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alisema tayari serikali imeingiza fedha zote hizo ambazo zinahitajika kukamilisha mradi huo.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Chunya wanapata maji ya uhakika serikali kupitia Wizara ya Maji imeanza usanifu wa kutafuta chanzo cha uhakika cha maji kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa eneo la Chunya Mjini.

Kasaka alisema hadi sasa upatikanaji wa maji katika wilaya hiyo uko kwa asilimia 30 na kwamba kwa kushirikiana na serikali wanaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali na fedha ili kukamilisha miradi ya maji inayojengwa na inayotarajiwa kujengwa.

"Wilaya yetu inapata maji kwa asilimia 30 hii ni kutokana na jiografia ya eneo hili kuwa kame lakini kukosekana kwa vyanzo vingi vya maji serikali imejitahidi kujenga miradi ya maji katika baadhi ya maeneo lakini bado tatizo lipo tunachokifanya kwa sasa ni wataalamu ambao ni Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuendelea kufanya utafiti kubaini vyanzo vingi vya maji ili vianze kujengwa," alisema.

Aliongeza kuwa miongoni mwa mafanikio katika kuhakikisha huduma ya maji inaboreshwa ni pamoja na kukamilika kwa mradi wa Matwiga ambao umekamilika kwa asilimia 100.

Mradi huo, alisema utaanza kutoa maji mapema mwezi Februari ambapo wakazi wa maeneo mbalimbali wanatufaika wakiwamo wa Makongolosi na Matundasi.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo wameishukuru serikali kwa kuendelea kuwasogezea karibu huduma ya maji na kwamba awali walikuwa wakitumia umbali mrefu kufuata maji ya visima kwa wawekezaji wa migodi ya dhahabu.

# Tulia ataka ajira mtaalamu wa mionzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SPIKA wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kupeleka haraka mtaalamu wa kitengo cha mionzi na kuongeza idadi ya wauguzi katika Kituo cha Afya cha Nzovwe, jijini Mbeya ili kuokoa maisha ya wanawake na watoto wanaokwenda kupata huduma za afya kwenye kituo hicho.

Dk. Tulia ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Nzovwe ambacho kitahudumia zaidi ya wananchi 20,000.

Kituo hicho cha afya kilijengwa na serikali miaka miwili iliyopita kwa gharama ya Sh. milioni 644 na kwamba mikakati iliyopo ni kuajiri mtaalamu wa mionzi ili kutoa huduma za afya kwa wahitaji wa huduma hiyo.

Uamuzi wa kuajiri mtaalamu wa mionzi kwenye kituo hicho ulitokana na ombi kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Kituo, Dk. Theobard Mutabiwa, ambaye alisema uhitaji ni mkubwa.

"Tunafurahia huduma za matibabu katika eneo letu la Nzovwe kwa sasa wananchi hawatumii gharama kufuata huduma maeneo mengine licha ya kwamba tunatarajia kupokea mashine ya mionzi, lakini hatuna mtaalamu ombi letu kwa serikali ni kupatiwa mtaalamu," alisema Dk. Mutabiwa.

Alisema licha ya uhitaji wa mtaalamu wa mionzi pia wanakabiliwa na uhaba wa wauguzi katika kituo hicho ambapo kwa sasa kuna wauguzi 30 na kwamba mahitaji ni 52 ili kukidhi haja kwa wateja 825 wakiwamo wajawazito 495, wanaohitaji huduma ya uzazi wa mpango 125 na wanaojifungua 38.

Dk. Tulia alisema atahakikisha suala hilo linafanyika haraka na kituo hicho kupata mtaalamu wa mionzi ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi.

"Niombe tu wakati serikali tukiendelea kuboresha miradi ya afya watumishi fanyeni kazi kwa wito katika kuwahudumia wananchi hususan wajawazito wanaofika kujifungua," alisema.

Alisema hatafurahishwa kusikia huduma zinazotolewa hazikidhi vigezo tunahitaji wagonjwa wafurahie huduma kulingana na matatizo yanayowaleta kupata huduma bora za afya kwa kuwa ndilo lengo la serikali.

Diwani wa Nzovwe, David Mwashilindi, alisema mradi huo umetokana na ombi lake kwa serikali kuhusu kujengewa kituo cha afya eneo hilo.

Alisema baada ya kuwasilisha ombi hilo, baraza la madiwani liliridhia kujenga kituo hicho cha afya kwa manufaa ya wakazi wa eneo hilo.





# Walimu watakiwa kufuata maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUTOKANA na tuhuma za udhalilishaji zinazomkabili Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Madungu, Kisiwani Pemba, kumdhalilisha mwanafunzi wake wa miaka 11 (jina linahifadhiwa), Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Pemba Muhamed Nassor Salim, amewataka walimu kufuata maadili ya kazi yao.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kutokana na tukio hilo linalomkabili mwalimu huyo mwenye umri wa miaka 25 ambaye anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumdhalilisha mwanafunzi wa darasa la tano.

Muhamed aliwataka walimu kufuata maadili ya kazi yao na kufuata sheria za utumishi kwa sababu wazazi wamejenga imani kwao kama walezi, hivyo kujiepusha na mazingira ambayo yanaweza kuleta tuhuma katika masuala ya udhalilishaji.

Aliwataka walimu kujitahidi kusimama kama walezi ili kushirikiana na serikali katika kuhakikisha watoto wapo salama bila ya kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Abdallah Hussein Mussa, alisema awali walipokea taarifa za malalamiko kutoka kwa mama mzazi wa mwanafunzi huyo akidai mtoto wake kudhalilishwa na mwalimu.

Alisema tukio hilo liliripotiwa Agosti 12, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni maeneo ya Shule ya Madungu. Mwalimu huyo anatuhumiwa kumwingilia kimwili mwanafunzi huyo ndipo Jeshi la Polisi lilipomkamata na kuanza kumhoji.

Kamanda Abdallah alisema Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi na utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kutii sheria bila shuruti na kuwaacha wanafunzi wasome ili kutimiza ndoto zao za maisha ya baadaye.

Naye mzazi wa mtoto huyo (jina linalihifadhiwa, alisema aligundua mtoto wake kufanyiwa kitendo cha udhalilishaji baada ya yeye akiwa na mtoto wake kusikiliza kipindi katika radio ambacho kilikuwa kikielimisha kuhusu masuala ya udhalilishaji.

"Baada kusikiliza kipindi mtoto wangu alianza kufunguka kwa kunieleza kuwa mama mwalimu mimi ameshanifanyia vitendo vya udhalilishaji shuleni wakati wanafunzi wakiwa washaondoshwa," alisimulia.

# Waziri ahimiza uongozi hutoka utotoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, amesema uongozi kwa wanawake lazima uanze katika ngazi za awali tangu watoto wakiwa shuleni ili kuwa viongozi mahiri wa baadaye.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano wa wadau na vijana wa kike wenye lengo la kuwezeshwa katika kuwania nafasi za uongozi Zanzibar, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Paul aliwataka vijana kutorudi nyuma licha ya changamoto mbalimbali wanazopitia katika kuwania nafasi za uongozi na kwamba hazimrudishi mtu nyuma bali zinampa nafasi ya kusonga mbele na kujiimarisha zaidi.

"Msiogope kuingia kwenye nafasi za uongozi na mara nyingi vijana wanakuwa waoga wanapoona kuna wanaume wamesimama kwenye majimbo. Msiogope na mnaposimama mtawapa changamoto wanaume na mwisho watatambua kama na nyie mna uwezo na elimu ya kuwania hizo nafasi," alisema.

Alisema nafasi za uongozi ziko nyingi na si lazima kwenye siasa na vijana wengi wamekuwa wakikimbilia kwenye uongozi wa siasa na kusahau sehemu zingine ambazo zimejaa wanaume.

Naibu waziri huyo alisema wanawake makini ni wale ambao hawaogopi kuingia kwenye nafasi hata kama kuna wanaume waliojitokeza kuwania hizo nafasi muhimu. Wao wanachangamkia nafasi hizo na kuingia kwenye kinyang'anyiro kuwania na kugombea nafasi za uongozi.

Alisema Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameonyesha mfano mzuri wa kuwainua wanawake kwa kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi, hivyo hakuna sababu ya wanawake kubaki nyuma kwa kuwa wana kigezo kizuri cha kuiga.

"Tunao mfano mzuri wa Mheshimiwa Rais wetu ametuinua sana wanawake kwa kututeuwa lakini jamii isiturudishe nyuma. Tutumie nafasi zetu kama wanawake na tusikubali kushindwa na wanaume katika kuwainua wanawake vijana ambao wanapaswa kusimama katika nafasi za uongozi," alisema.

Alisema TAMWA ni taasisi inayosaidia wanawake na vijana kwa muda mrefu ikiwainua katika masuala mbalimbali ikiwamo ya kudai haki za wanawake, kupambana na udhalilishaji, kuwania nafasi za uongozi, pia kuwainua na kuwajengea uwezo wa nafasi za uongozi ikiwamo vijana.

Alisema amefurahishwa na kuiona TAMWA ikifanya kazi zake kwa ufanisi hasa katika kuwachukua vijana na kuanza kuwapa elimu ya kujiamini na kujitambua ili kuwania nafasi za uongozi mapema kabla ya kumaliza vyuo na muhimu kuanza kupewa elimu mapema ni jambo zuri na la busara zaidi.

"Ni muhimu nafasi hizi za uongozi kugombewa kuanzia kwa vijana shuleni na ukija katika jamii unaendeleza kwa kuwa tayari umeshapata uzoefu, hivyo tujitahidi katika kuwainua vijana na vijana mhamasike," alisema.

Naye Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, alisema wazee wanamalizia umri wao katika nafasi zao, hivyo zinahitaji kujazwa na vijana.

"Vijana mnapaswa kujituma zaidi ili kuchukua nafasi za uongozi na hivi sasa wazee wanazeeka na kuondoka na nafasi hizi zinahitaji kujazwa. Ninyi ndio mtatakiwa kuchukua hizo nafasi na hasa kwa kuzingatia hivi sasa tuna nafasi nzuri kwa kuwa Rais wetu wa Tanzania ni mwanamke," alisema Dk. Mzuri.

Akitoa ushuhuda wake, Dk. Mzuri alisema alianza kupenda kuandika na kutoa taarifa zinazowahusu wanawake na vijana kabla ya kujiunga na TAMWA na mwisho akajikuta amewasaidia wanawake.

Kuhusu masuala ya wanawake na uongozi, Dk. Mzuri alisema kupitia TAMWA imetumia nafasi ya kuwajengea uwezo wanawake ili kujitokeza kushiriki katika kuchukua fomu za nafasi za udiwani, uwakilishi na ubunge ili waingie katika vyombo vya kutunga sheria kupitia kwenye majimbo yao na si kutegemea nafasi za viti maalumu ambazo kwa muda mrefu zinaonekana haziwasaidii wanawake katika kujiimarisha na kuingia katika ushindani.

Alisema wizara ya jinsia ina wajibu wa kuwasaidia wanawake katika uongozi na kwa kusaidiana na wanaharakati mbalimbali wanaweza kuwainua wanawake wenzao ili wawe wengi kwenye uongozi.

"Kwa miaka mingi nguvu, uwezo na majukumu ya wanawake ulikua ukibezwa lakini kwa sasa wanawake wananguvu ya kufanya mambo makubwa yanayostahiki," alisema.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul (wa pili kulia), akizungumza katika mkutano wa wadau na vijana wa kike kuhusu kuwawezesha wanawake kuwa viongozi ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watakiwa kuwajibika kwa maslahi ya taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa kamati ya kitaifa ya kuratibu utekelezaji wa mpango wa kurekebisha hoja za ukaguzi wa Shirika la Kimataifa la Bahari Duniani (IMO) wametakiwa kuwajibika vyema katika jukumu walilokabidhiwa ili kufanikisha lengo lililokusudiwa.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wajumbe hao kupitia kikao cha mashauriano kilichofanyika katika ukumbi wa wizara hiyo, Kisauni.

Alisema wizara kwa kutambua umuhimu wa hitaji la kuimarisha sekta ya usafiri baharini, imeamua kuunda kamati hiyo ambayo imeshirikisha mjumbe mmoja kutoka kila taasisi husika.

Suala la utekelezaji wa mpango kazi wa masahihisho, alisema ni miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na serikali zote mbili katika kutimiza wajibu na majukumu ya nchi kwa jumuiya ya kimataifa katika kutatua changamoto hizo.

"Kuundwa kwa kamati hii, pamoja na mambo mengine, kumelenga kusaidia utekelezaji wa mpango kazi wa masahihisho kwa lengo la kuimarisha usalama wa baharini na ulinzi wa mazingira ya bahari ya nchi yetu na ulimwenguni kwa ujumla," alisema Dk. Khalid.

Alisema uongozi wa wizara una imani kubwa na watendaji waliochaguliwa katika kamati hiyo kutokana na weledi na ujuzi hivyo wataifanikisha kazi hiyo kwa moyo wa kizalendo.

Aidha, Dk. Khalid alisema hoja hizo zimegawanyika katika makundi sita zikijumuisha sheria na kanuni, mafunzo na utaalamu, mifumo na miongozo ya kazi, vifaa na vitendea kazi, sera, mipango na mikakati pamoja na tathmini na ufuatiliaji wa utendaji.

Waziri huyo aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kuhakikisha ifikapo Desemba, mwaka huu, wawe wamekamilisha ripoti maalum itakayokuwa na mpango kazi pamoja na bajeti ya utekelezaji wake.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini, Sheikh Ahmed Mohamed, alisema kupitia kamati hiyo ya wataalamu iliyoundwa, mamlaka inakusudia kurekebisha changamoto zote zilizojitokeza ili muda ukifika kwa ajili ya ukaguzi ikamilike kwa ufanisi.

# HABARI PICHA



Viongozi na makarani wa sensa wakiingia kwenye makazi ya Rais Samia Suluhu Hassan, Chamwino, Ikulu, mkoani Dodoma jana, kuhesabu familia yake. Mstari wa mbele (kutoka kushoto) ni Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule na Kamishna wa Sensa Tanzania Bara, Anne Makinda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akihojiwa na Karani wa Sensa, Anthony Mlegi, wakati akihesabiwa katika makazi yake, wilayani Magu, mkoani Mwanza jana. **PICHA: HAPPY SHAYO**



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akifurahia jambo na karani wa Sensa ya Watu na Makazi, Faith Buruhani, wakati wa akihesabiwa katika makazi yake, Msasani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ADAM MZEE WA CCM**



Karani wa Sensa ya Watu na Makazi, Stella Kisenha, akiwahoji wakazi wa Goba Tegeta A, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe Mama Mbonimpaye Mpango, wakizungumza na karani wa sensa, Isack Mgosho, walipokuwa wakihesabiwa katika makazi yao, Chanika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**



Mbunge wa Jimbo la Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (kushoto), akihojiwa na Karani wa Sensa ya Watu na Makazi, Robert Method katika Kijiji cha Kwemhanya, wilayani humo jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwemhanya, Weston Robert. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Msumbiji yapatiwa msaada dola milioni 300

**MAPUTO,** MSUMBIJI

BENKI ya Dunia imeipatia Msumbiji msaada wa dola milioni 300 kama moja ya kuashiria kurejea kwake nchini humo baada ya miaka sita ya kusitisha msaada wake wa kifedha kutokana na kashfa ya deni ambayo haikuwekwa wazi.

Waziri wa Fedha wa Msumbiji, Max Tonela, alibainisha jana kuwa pesa hizo zitatumiwa kufadhili miradi ya miundombinu ili kusaidia kuimarisha uchumi na kuboresha hali ya maisha katika nchi hiyo.

Wakati wa hafla ya utiaji saini wa msaada huo Tonela alieleza kwamba hiyo ni bajeti ya kwanza ya msaada ambayo wanatumai kuiona katika miaka mitatu ijayo.

Pia ilielezwa kuwa makubaliano hayo yanafuatia mkataba wa dola milioni 456 na Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF) uliosainiwa mwezi Mei ulioashiria kuwa Msumbiji imerudi kuaminiwa na wafadhili baada ya kashfa ambayo ilisababisha mzozo mbaya wa kiuchumi tangu taifa hilo lijipatie uhuru kutoka kwa Ureno zaidi ya miongo minne iliyopita.

Kwa mujibu wa VOA serikali ya nchi hiyo ilichukua mikopo ya siri yenye thamani ya dola bilioni mbili mwaka wa 2013 na 2014 kutoka kwa benki za kimataifa ili kununua meli za uvuvi na meli za ukaguzi. **VOA**

## Mwandishi auawa kwa risasi Mexico

**GUERRERO,** MEXICO

MWANDISHI mmoja wa habari ameuawa kwa kupigwa risasi huko kusini mwa Mexico kipindi kifupi baada ya kusambaza mtandaoni picha ya wanafunzi 43 waliotoweka katika mazingira tatanishi miaka nane iliyopita.

Ofisi ya mwendesha mashtaka nchini humo jana ilisema, mwandishi huyo Fredid Roman, ambaye anasambaza kazi zake kwenye kurasa mbalimbali za mitandao ya kijamii na mwandishi wa gazeti moja la Mexico, alikutwa amekufa ndani ya gari lake katika mji wa Chilpancingo, mji mkuu wa jimbo la Guerrero.

Kwa mujibu wa rekodi za Shirika la Waandishi wa Habari wasio na mipaka (RSF) kwa mwaka huu pekee waandishi wa habari 12 wameuawa nchini Mexico, huku vyanzo vingine vikisema 15 au 16.

Ilielezwa kuwa kisa cha wanafunzi 43 kutoka Guerrero, ambao walitoweka mwaka 2014 baada ya kuamuru basi kuelekea kwenye maandamano, kinachukuliwa kuwa moja ya tukio baya zaidi la haki za binadamu katika historia ya Mexico. **DW**

# Watoto 1,000 wauawa vita Russia na Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF) linasema takriban watoto 1,000 wa Ukraine wamethibitishwa kuuawa au kujeruhiwa tangu Russia iivamie Ukraine miezi sita iliyopita.

UNICEF ilisema jana kwamba hesabu yake ya jumla ya watoto 972 waliouawa inajumuisha wale ambao wamethibitishwa na Umoja wa Mataifa (UN) na kusema idadi ya kweli huenda ikawa kubwa zaidi.

**Kwa mara nyingine kama katika vita vyote, maamuzi ya kutojali watu wazima yanaweka watoto katika hatari kubwa, hakuna operesheni za kutumia silaha za aina hiyo ambazo hazisababishi watoto kudhuriwa**

Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF Catherine Russell, alisema vifo vingi vya watoto hao vilisababishwa na silaha za milipuko.

"Kwa mara nyingine kama katika vita vyote, maamuzi ya kutojali watu wazima yanaweka watoto katika hatari kubwa, hakuna operesheni za kutumia silaha za aina hiyo ambazo hazisababishi watoto kudhuriwa," alisema Russell.

Aliongeza kuwa mbali ya watoto waliouawa au kujeruhiwa katika machafuko hayo, pia karibu kila mtoto nchini Ukraine alikabiliwa na matukio yenye kuhuzunisha na wale wanaokimbia machafuko wako katika hatari kubwa ya kutengana na familia, machafuko, unyanyasaji, kudhulumiwa kingono na usafirishaji haramu.

Aidha, alieleza kwamba shirika lake linakadiria kuwa shule moja kati ya 10 nchini Ukraine ziliharibiwa au kubomolewa katika vita.

Pia UNICEF ilitoa wito wa kumaliza matumizi ya silaha za milipuko katika maeneo yanayokaliwa na watu wengi, ikiwa ni pamoja na mashambulizi dhidi ya majengo ya raia na miundombinu. **VOA**



Mzazi akipita na mwanawe nje ya jengo lililoharibiwa vibaya kutokana na vita inayoendelea Ukraine. **PICHA: MTANDAO**

# Nyaraka za siri zakutwa kwa Trump

**FLORIDA,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imekuta zaidi ya nyaraka 300 zenye alama ya siri nzito za serikali kwenye makazi ya Rais wa zamani Donald Trump yaliyoko Florida.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na gazeti la New York Times, nyaraka zilizokutwa ni za shirika la ujasusi (CIA), usalama wa taifa (NSA) na Shirika la Upelelezi wa Ndani (FBI).

Ilisema fungu la kwanza la zaidi ya nyaraka 150 zilizokuwa na alama ya siri ziligunduliwa na taasisi ya kitaifa ya utunzaji wa nyaraka mwezi Januari.

Pia ilieleza kuwa wasaidizi wa Trump waliipatia wizara ya sheria seti ya pili mwezi Juni, na seti ya tatu iligunduliwa na FBI walipovamia na kupekua makazi ya Trump mapema mwezi huu.

Hata hivyo wizara hiyo pamoja na wawakilishi wa Rais huyo wa zamani hawakuwa tayari kuzungumzia mara moja ugunduzi huu wa karibuni ulipotafutwa kutoa ufafanuzi.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa mapema juzi, Trump aliomba mahakama ya shirikisho kuwazuia FBI kwa muda kupitia nyaraka zilizokuwa na alama ya siri nzito ilizozikamata Agosti 8 kwenye makazi yake ya Mar-a-Lago hadi kutakapoteuliwa msimamizi maalumu wa kusimamia suala hilo.

Ilielezwa kuwa hoja ya Trump, iliyowasilishwa katika mahakama ya shirikisho huko Florida, pia iliitaka wizara ya sheria ya Marekani kumpatia ankara inayoonyesha kwa kina zaidi ya nyaraka zilizokamatwa na FBI kwenye nyumba yake ya Mar-a-Lago na kuwataka wachunguzi hao kurudisha vitu vyovyote ambavyo haviko kwenye kibali cha uchunguzi wao.

Taarifa hiyo ilisema msimamizi maalumu mara nyingine anaweza kuteuliwa katika kesi nyeti zaidi ili kupitia nyaraka zinazoshikiliwa na kuhakikisha wachunguzi hawapitii taarifa za upendeleo, wakati FBI walipokuwa wakipekua nyumba za Trump, ambapo mawakili wake wa zamani Michael Cohen na Rudy Giuliani waliomba kuteuliwa kwa msimamizi huyo.

Hakimu Bruce Reinhart, kutoka West Palm Beach aliyeidhinisha kibali cha upekuzi kwenye makazi ya Trump ya Mar-a-Lago, anaangazia iwapo anaweza kuiagiza wizara ya sheria kutoa nakala iliyorekebishwa ya hati ya kiapo inayoonyesha ushahidi wa sababu za kupekuliwa kwa nyumba ya Trump.

Vile vile ilielezwa kuwa kukamatwa kwa nyaraka hizo ni sehemu ya uchunguzi wa FBI kuhusiana na iwapo Trump aliondoa nyaraka kinyume cha sheria wakati alipoondoka madarakani Januari 2021 baada ya kushindwa kwenye uchaguzi na Rais Joe Biden kuingia mamlakani.

Taarifa pia ilisema kwamba Trump na washirika wake walilalamika mbele ya vyombo vya habari kwamba upekuzi huo ulichochewa kisiasa. **DW**

HABARI MICHEZO

# KIM MATUMAINI STARS, UGANDA, ZANZIBAR HEROES ZIKIJIPIMA LEO

**Saada Akida, Dar na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen, akisema ana matumaini makubwa ya kushinda mchezo wao dhidi ya Uganda nyumbani ili kurahisisha kazi kwenye mchezo wa marudiano ugenini, wapinzani wao hao wametua visiwani Zanzibar na leo watacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), kujiandaa na mechi hiyo.

**Stars na Uganda zitashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii kusaka matokeo ya kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika nchini Algeria baadaye mwaka huu.**

Tayari Stars ipo kambini tangu juzi, lakini haina ratiba yoyote ya mechi ya kirafiki wakati huu ikijiandaa na michezo hiyo miwili, nyumbani na ugenini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kim alisema wachezaji wote aliowaita katika kikosi chake akiwamo, Tepsie Evance kutoka Azam FC, aliyemwongeza kikosini, tayari wameanza mazoezi na wanaendelea vizuri kwa ajili ya mchezo huo wa Jumapili.

Alisema mazoezi wanafanya mara moja na morali ya wachezaji iko juu na wana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika mchezo wa kwanza watakaocheza nyumbani.

"Kikosi kimeingia kambi jana (juzi), na leo tumeanza mazoezi rasmi kuelekea mchezo wetu dhidi ya Uganda, tunatakiwa kushinda mchezo huu ili kuhakikisha mechi ya marudiano isiwe ngumu kwa sababu tutakuwa ugenini," alisema Kim huku akibainisha mchezo huo utakuwa mgumu.

Kwa upande wa Uganda, tayari imetua visiwani Zanzibar tangu juzi ikitokea Ethiopia kwenye mechi nyingine ya kirafiki na leo, Jumatano saa 1:00 usiku itashuka katika Uwanja wa Amaan kuivaa Zanzibar Heroes katika mchezo wa kirafiki maalum kwa ajili ya maandalizi ya kuivaa Taifa Stars.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), tayari limetangaza viingilio vya mchezo huo ambapo kwa VIP itakuwa ni Sh. 5,000, 'Wings' Sh. 3,000, huku Urusi mzungo ikiwa ni Sh. 2,000 tu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa mchezo huo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ZFF, Ali Bakari 'Cheupe', alisema maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na Uganda tayari wameshaingia visiwani Zanzibar, huku Zanzibar Heroes ikiendelea na mazoezi.

"Tunaendelea na Mazoezi kwani huu mchezo wa kirafiki kwetu sisi ni muhimu ili kuwapa furaha Wazanzibar kwa sababu timu ya Zanzibar haijacheza mchezo wowote ikiwa hapa nyumbani ukiondoa michuano ya Cecafa ambayo kwa mara ya mwisho ilichezwa Uganda," alisema.



Kiungo wa Taifa Stars, Jonas Mkude, akikokota mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika juzi katika viwanja vya JK Park jijini Dar es Salaam kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Uganda itakayopigwa Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TPLB yatoa neno ushindani Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara imemalizika huku Simba ikiwa ni timu pekee ambayo haijaruhusu bao lolote mpaka sasa.

Mpaka sasa jumla ya mabao 40 yamefungwa, huku kila raundi yakifungwa mabao 20, Simba ikiwa kinara wa kufunga mabao mengi kuliko timu nyingine, kutokana na kupachika mabao matano. Simba imecheza mechi mbili, ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Geita Gold na 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Bodi ya Ligi nayo imeonyeshwa kuridhishwa na mwanzo mzuri wa ligi hiyo, kutokana na ushindani mkali uliojionyesha kwenye mechi za mwanzo tu.

"Tumeanza vizuri malengo tuliojiwekea, ni kama vile yameanza kutekelezeka, ikiwamo kushuhudia burudani na ushindanni, timu zote zilizocheza raundi mbili za mwanzo, zimeonyesha ushindani mkubwa, pia tumepata burudani kutoka kwao.

"Imethibitika kwa namna ambavyo timu zilivyopambana kupata ushindi na hata zile zilizofungwa, zimeonekana kupambana sana, na ndiyo maana mpaka sasa ni timu moja tu ambayo haijaruhusu bao ambayo ni Simba, kwa hiyo ligi imeanza kwa upinzani mkali," alisema Karim Boimanda ambaye ni Ofisa Habari wa bodi hiyo.

Alisema kuwa pia wameanza vema upande wa usimamizi wa michezo yenyewe, wamekuwa wakifanya maandalizi ya maofisa wanaokwenda kusimamia michezo kama vile waamuzi na makamisaa.

Wakati msimu huu kila raundi iliyochezwa ikizalisha mabao 20, rekodi zinaonyesha kuwa msimu uliopita mpaka raundi ya pili ilipomalizika, ni mabao 22 tu yalikuwa yamefungwa.

Yalipatikana kwa raundi ya kwanza kupachikwa mabao 10, na ya pili mabao 12.

## Singida Big Stars yabadili kambi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Singida Big Stars, imefanya mabadiliko ya kambi yake katika kipindi hiki cha mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa, ambapo sasa inatarajia kutua jijini Mwanza leo badala la Jiji la Kitalii, Arusha.

Ligi Kuu Tanzania Bara inasimama kwa takriban wiki mbili kupisha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kucheza mechi mbili za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Uganda nyumbani na ugenini, hivyo timu za ligi kuu kutumia kipindi hiki kujiimarisha zaidi kabla ya mtifuano huo kurejea Septemba 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mkoani Singida, Msemaji wa timu hiyo, Hussen Masanza, alisema awali kambi hiyo walipanga waiweke mkoani Arusha, lakini wamebadili ratiba hiyo na sasa watakuwa jijini Mwanza.

"Tunakwenda kuweka kambi Mwanza badala ya Arusha tunataka wachezaji wetu wazoee hali ya hewa mapema mkoani Mwanza kwa kuwa tutacheza michezo miwili ya Ligi Kuu ukiachana na ule ambao tutaucheza nyumbani Septemba 11, mwaka huu na timu ya Dodoma Jiji," alisema Masanza.

Alisema wakiwa Mwanza watacheza mchezo wa kwanza wa kirafiki Agosti 27, mwaka huu dhidi ya timu ya Pamba FC katika Uwanja wa CCM Kirumba.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi, Mathias Lule, alisema: "Kwa sasa ninaendelea kuinoa timu ili iwe na muunganiko mzuri, kuhusu ushindani wa namba kwa sasa ni mapema kuuzungumzia kwa kuwa nina timu yenye wachezaji wenye viwango vya hali ya juu," alisema Lule.

## KMKM yapania Ngao ya Jamii

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI akitarajia kukiongoza kikosi chake Jumapili wiki hii kuivaa Kipanga FC kwenye mechi ya Ngao ya Jamii, maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2022/23, Kocha Msaidizi wa Timu ya KMKM, Ame Msimu, amesema matarajio yao ni kuhakikisha anaingia msimu mpya kwa kubeba taji hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msimu alisema kwa sasa wachezaji wao wanaendelea na mazoezi katika Uwanja wa Amaan utakaopigwa mchezo huo, na kwamba kikubwa ni kufuata mpangilio mzuri wa timu.

Hata hivyo, kuelekea mchezo huo utakaopigwa Jumapili majira ya saa 10 alasiri, Maafande wa Kipanga nao jana walionekana wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 12 asubuhi.

## ZISIKUPITE

### GORDON ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea ina imani kuwa inaweza kufikia makubaliano ya kumnunua mshambuliaji wa Everton, Anthony Gordon, 21, wiki hii. ***(Times)***

### AUBAMEYANG NA CHELSEA

CHELSEA wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Pierre-Emerick Aubameyang, 33, kwa mkataba unaodhaniwa kuwa wa thamani ya kati ya pauni milioni 15 na pauni milioni 25. ***(Sky Sports)***

### NANE KUONDOKA CHELSEA

CHELSEA wako tayari kuruhusu wachezaji nane wa ziada kuondoka katika dirisha hili baada ya West Ham kukubali dili la kumsajili beki wa Italia, Emerson Palmieri, 28. ***(Express)***

### UNITED WAKOMAA NA JONG

MAOFISA kutoka Manchester United wanatazamiwa kusafiri hadi Barcelona katika juhudi za mwisho za kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(De Telegraaf via Mail)***

### SARR MKATABA MPYA

KLABU ya Watford haitakubali ofa yoyote kwa mshambuliaji wa Senegal, Ismaila Sarr, 24 na wako tayari kumpa mchezaji huyo mkataba mpya wa muda mrefu baada ya Aston Villa kushindwa kumnunua. ***(Mirror)***

### PEDRO AITESA WATFORD

WATFORD pia hawajakubali ofa ya Newcastle United ya pauni milioni 25 kwa fowadi wa Brazil, Joao Pedro, 20. ***(Telegraph)***

### ANTONY SAFI UNITED

MANCHESTER United wako tayari kukamilisha usajili wa fowadi wa Ajax, Antony, 22, ndani ya wiki ijayo, baada ya kuripotiwa kuafikiana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Sun)***

### JAMES AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Leeds United na Wales, Daniel James, 24. ***(Alan Nixon, via Leeds Live)***

### ALONSO BASI BARCA

BARCELONA wanamtazama beki wa kushoto wa Celta Vigo, Javi Galan, 27, kama mbadala wa mlinzi wa Chelsea, Marcos Alonso, 31, kwa sababu uhamisho wa kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania unazidi kuwa mgumu. (***Helena Condis Edo via Twitter)***


### KALAJDZIC KUTUA WOLVES

KLABU ya Wolves imekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa VfB Stuttgart na Austria, Sasa Kalajdzic, 25, lakini mazungumzo kati ya klabu hizo mbili bado yanaendelea kuhusu mchezaji huyo. ***(Mail)***

### TRAPP AIVUTIA UNITED

MANCHESTER United pia wanavutiwa na mlinda mlango wa Eintracht Frankfurt na Ujerumani, Kevin Trapp, 32. ***(Sky Sports via Football Daily)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG FURAHA TUPU KUITUNGUA LIVERPOOL

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amekiri furaha yake ya kupata ushindi wake wa kwanza kama kocha wa Manchester United wakati timu yake iliposhinda mabao 2-1 dhidi ya Liverpool, Jumatatu usiku.

**Washambuliaji Jadon Sancho na Marcus Rashford waliwafanya vijana hao wa Old Trafford kuongoza kwa mabao 2-0 na Mohamed Salah akafunga bao la kichwa kipindi cha pili, lakini halikutosha na kuwafanya Man United kuondoka na pointi zote tatu.**

Wakiwa wametoka kupoteza mechi zao mbili za ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya Brighton na Brentford - Ten Hag alisisitiza kwamba anabakia kuzingatia kile kinachofuata.

> Sidhani kama wanaweza kuleta kila wakati kama leo, lakini unaweza kuwa na nguvu, umakini...

Aliiambia BBC Sport: "Ushindi wa kwanza bila shaka unaleta furaha nyingi. Tulikuwa na mwanzo mgumu, lakini nina furaha sana hasa kwa mashabiki na dhidi ya Liverpool.

"Nilifurahia tangu dakika ya kwanza, lilikuwa pambano kubwa sana. Timu zote mbili zilifanya vizuri na ulikuwa usiku mzuri, haswa kwa mashabiki wa Manchester United.

"Tulikuwa na pre-season nzuri sana, tulicheza kwa kiwango kizuri, kisha tukawa na mapungufu. Haikuwa rahisi kukabiliana na hilo, lakini unapoanza mchakato unagundua tabia za watu binafsi na timu na mimi.

"Hakika hatukuridhika baada ya kupoteza haswa dhidi ya Brentford. Leo umeona majibu, huo ndio mtazamo.

"Sidhani kama wanaweza kuleta kila wakati kama leo, lakini unaweza kuwa na nguvu, umakini kila wakati, roho ya mapigano na kila wakati mahitaji hayo ni msingi wa timu kushinda michezo."

Kinachofuata kwa United ni safari ya kuelekea Southampton Jumamosi huku wakijaribu kupata uimara zaidi chini ya kocha wao huyo mpya.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,025,1


MECHI KALI
LEEDS
VERSUS
BARNSLEY
1 | 1.26
X | 5.45
2 | 10.09

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PULISIC HUENDA AKABAKI CHELSEA



**LONDON** England

CHRISTIAN Pulisic huenda akabaki kuwa mchezaji wa Chelsea baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili la sasa, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani, amekuwa akihusishwa na klabu za Manchester United na Newcastle United katika wiki za hivi karibuni baada ya kuanza katika mechi 13 pekee za Ligi Kuu England msimu uliopita.


Pulisic ni miongoni mwa wachezaji wasiofurahishwa na mbinu na mawasiliano ya kocha Thomas Tuchel.

Wachezaji wenzake, Romelu Lukaku na Timo Werner, tayari wameondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto baada ya kuhangaika chini ya Tuchel msimu uliopita.

Hata hivyo, vyanzo vimeiambia 90min kwamba, Chelsea wanasita kukubali ofa za mkopo kwa Pulisic, huku wakijua ubora wa mchezaji huyo licha ya kukosa muda wa kucheza na matatizo ya majeraha.

Inafahamika kuwa Chelsea bado inawawinda mshambuliaji wa Barcelona, Pierre-Emerick Aubameyang, winga wa Everton, Anthony Gordon na kiungo mwingine. Iwapo Chelsea itaweka malengo yao yote, kuondoka kwa Pulisic itakuwa rahisi kidogo.

Hata hivyo, 'The Blues' hao pia wanataka kuwaondoa wachezaji kadhaa msimu huu, huku Hakim Ziyech, Callum Hudson-Odoi na Michy Batshuayi, wote wakiwa miongoni mwa wachezaji wanaotarajiwa kuondoka hapo Stamford Bridge.



## *Arsenal yajipanga kumsajili Neto*

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal inawania kumnunua Pedro Neto, ambaye wamemweka kama kipaumbele chao kikubwa kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la majira haya ya joto.

Mapema mwezi huu, Arsenal ilionyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, huku pia akiwaniwa na Chelsea na Manchester United.

Sasa inaelewaka kwamba, Arsenal wanapanga ofa kwa Neto, ambaye wamekuwa mashabiki wake kwa muda mrefu.

Arsenal wanataka mchezaji mpya wa upande wa kulia, jambo ambalo lilithibitishwa na ombi lao mapema msimu wa majira ya joto kwa Raphinha, ambaye aliamua kuhamia Barcelona.

Neto alirejea kutoka kwenye jeraha baya la goti mapema mwaka huu, na baada ya kuthibitisha utimamu wake aliingia mkataba mpya wa muda mrefu pale Molineux.

# 118,259/-

# MJASIRIAMALI ALAMBA MIL. 5/- JACKPOT BONASI YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mwongolo Majengo Mapya wilayani Kahama, Shinyanga, Ruben Kessy, ameshinda jumla ya Sh. 5,175,798, kwenye Jackpot bonasi ya SportPesa.

**Akizungumza baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi katika ofisi za SportPesa, Oysterbay, Dar es Salaam juzi, Ruben alisema alianza kucheza na SportPesa miaka minne iliyopita baada ya kushawishiwa na rafiki yake.**

"Mimi nilianza kucheza na SportPesa mwaka 2018, baada ya kuona rafiki yangu, jina sitomtaja, akicheza na kushinda mara kwa mara. Wakati ule mimi nilikuwa natumia simu ya kitochi, hivyo ilimlazimu rafiki yangu kunifundisha kwa kutumia USSD," alisema.

Ruben ambaye ni mjasiriamali wa kilimo na ufugaji, anasema katika safari yake ya kucheza na SportPesa ameshawahi kushinda mara kadhaa katika bashiri za kawaida na mara moja Jackpot bonasi ya timu 10.

"Unajua nilishawahi kushinda 90,000, 100,000 na 600,000 katika mikeka ya kawaida na Sh. 220,000 katika Jackpot bonasi ya mechi 10," alisema Ruben.

Akizungumzia mkeka wake wa Jackpot ya katikati ya wiki alioshinda, Ruben alisema aliuona mkeka huo Jumatatu ya Agosti 15 na kisha aliuchambua na kuuweka siku hiyo hiyo.

"Kwanza nikiri nilipoziona mechi za Jackpot hii ya katikati ya wiki, sikuwa na uhakika mkubwa wa kushinda. Ila nilijitahidi kuziangalia kidogo timu zilizokuwapo kwa kutumia simu yangu na kucheza kama uchambuzi wangu nilivyouona."

Ruben anaendelea kusema baada ya kubet hakuufuatilia mkeka wake ila anachokumbuka ni Agosti 18 alilala majira ya saa nne usiku. Baadaye majira ya saa saba aliamka kwenda msalani na ndipo aliposhika simu na kuona meseji ya ushindi.

"Kwa kweli baada ya kuona sms ya kunipongeza sikupata tena usingizi. Nilikaa kitandani mpaka kunakucha na kusubiria hatima ya kile kitakachofuata maana nilikuwa na furaha sana.

"Nilimshirikisha rafiki yangu na kumweleza kwamba nimeshinda Jackpot ya SportPesa, lakini sikumwambia kiwango halisi. Baada ya hapo nilipiga namba za huduma kwa wateja SportPesa na kuulizwa maswali machache kisha baada ya dakika tano nilipigiwa simu tena na kupewa maelekezo nifike ofisi za SportPesa makao makuu Dar es Salaam, na kisha nikafuata utaratibu wote."

Ruben anahitimisha kwa kuwaasa Watanzania kutumia fursa ya kubashiri wakiwa makini kwani inawapa nafasi kubwa ya kushinda. Ninawaasa Watanzania wenzangu wajitahidi kucheza kwa umakini kwa kuchambua timu kwa undani.

Naye Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Ruben kwa kushinda Jackpot Bonasi na kuwataka Watanzania kucheza Jackpot zote yaani hii ya katikati ya wiki na Supa Jackpot ambayo inachezwa mwishoni mwa wiki. Kwa wiki hii Jackpot ya katikati ya wiki imesimamia Sh. 323,022,530 na Supa Jackpot ikiwa 1,025,118,259/-.




Mshindi wa Jackpot Bonasi, Ruben Kessy kutoka Kahama mkoani Shinyanga, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 5, baada ya kukabidhiwa juzi kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Minziro afunguka Mjapan wa Geita Gold dimbani*

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amesema wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha vibali vya nyota wao, Shinobu Sakai raia wa Japan, tayari kwa kuanza kumtumia kwenye mechi za Ligi Kuu na mashindano mengine.

Geita Gold ambayo inajiandaa na mashindano ya kimataifa ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu zilizosajili nyota wa kimataifa kwa lengo la kuleta ushindani.

Akizungumza na Nipashe jana, Minziro alisema, anaimani kubwa na Mjapan wake pindi atakapoanza kuitumikia timu hiyo, na kudai kuwa wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha vibali vyake vya kufanya kazi nchini ili kuanza kutumika.

"Tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha vibali vya mchezaji wetu Shinob, hakuweza kucheza mechi za awali kwa kuwa hakuwa na kibali cha kazi na makazi, hivyo tunakamilisha utaratibu ili aweze kucheza.

"Ninamatumaini makubwa akianza kucheza kikosi kitakuwa kizuri pale atakapozoeana na wachezaji wenzake, lengo letu tunahitaji kuwa na kikosi bora cha ushindani msimu huu kuliko ulivyokuwa msimu uliopita," alisema Minziro.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/08/22 | 17:00 | Blackpool vs Bristol City | 2.28 | 3.19 | 3.19 |
| 02. 27/08/22 | 17:00 | Cardiff vs Preston | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 03. 27/08/22 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 04. 27/08/22 | 17:30 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 2.33 | 3.53 | 2.84 |
| 05. 27/08/22 | 19:30 | Juventus vs Roma | 2.31 | 3.19 | 3.14 |
| 06. 27/08/22 | 19:30 | Cremonese vs Torino | 2.99 | 3.34 | 2.32 |
| 07. 27/08/22 | 21:45 | Spezia vs Sassuolo | 2.99 | 3.39 | 2.29 |
| 08. 27/08/22 | 22:00 | Lens vs Rennes | 2.44 | 3.36 | 2.76 |
| 09. 28/08/22 | 01:00 | Fluminense vs Palmeiras | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 10. 28/08/22 | 14:00 | Nantes vs Toulouse | 2.40 | 3.27 | 2.88 |
| 11. 28/08/22 | 14:30 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 12. 28/08/22 | 14:30 | Hannover vs Greuther Furth | 2.79 | 3.39 | 2.43 |
| 13. 28/08/22 | 15:15 | FC Lugano vs St. Gallen | 2.45 | 3.49 | 2.69 |
| 14. 28/08/22 | 16:00 | Aston Villa vs West Ham | 2.37 | 3.24 | 2.99 |
| 15. 28/08/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Newcastle | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 16. 28/08/22 | 16:00 | Nice vs Marseille | 2.48 | 3.33 | 2.73 |
| 17. 28/08/22 | 16:00 | Troyes vs Angers | 2.53 | 3.18 | 2.78 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 24 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1761 | Shijiazhuang vs Hangzhou NG | 5.52 | 3.79 | 1.53 |
| 13:00 | 1398 | Gold Coast United vs Peninsula Power | 2.94 | 3.77 | 2.03 |
| 13:00 | 4947 | Tokyo Verdy vs Tokushima Vortis | 2.71 | 3.00 | 2.51 |
| 14:30 | 3602 | Guangzhou Evergrande vs Dalian Aerbing | 3.53 | 3.38 | 1.92 |
| 14:45 | 1774 | Young Lions vs Tampines | 7.69 | 6.31 | 1.23 |
| 15:00 | 1127 | Rukh Vinnyky vs FC Metalist Kharkiv | 2.12 | 3.14 | 3.24 |
| 15:15 | 1271 | Kuching FA vs Selangor Pkns | 1.67 | 3.64 | 4.42 |
| 16:00 | 1161 | Persija Jakarta vs Persita Tangerang | 1.78 | 3.38 | 4.11 |
| 17:20 | 2028 | Umm-Salal SC vs Al-Sailiya SC | 1.96 | 3.49 | 3.29 |
| 18:00 | 1002 | Mamelodi Sundowns vs Stellenbosch | 1.54 | 3.66 | 6.42 |
| 18:00 | 3068 | Malisheva vs KF Ferizaj | 2.24 | 3.38 | 2.79 |
| 18:00 | 4208 | KF Drenica Skenderaj vs KF Gjilani | 3.10 | 3.60 | 2.00 |
| 18:30 | 2164 | Ismaily SC vs Eastern Company SC | 2.25 | 3.00 | 3.35 |
| 19:00 | 1009 | HJS Akatemia vs FC Jazz | 1.93 | 4.02 | 2.99 |
| 19:00 | 1213 | Grankulla Ifk vs EPS | 1.70 | 4.02 | 3.82 |
| 19:00 | 1218 | Vjs vs Tampere United | 2.51 | 3.83 | 2.27 |
| 19:00 | 1664 | FC Ilves-Kissat vs Kaapo Kaarina | 1.26 | 5.87 | 7.25 |
| 19:00 | 3210 | FC Helsingor vs Lyngby | 3.54 | 3.74 | 1.82 |
| 19:00 | 3948 | Racing Club (URU) vs CA Atenas De San Carlos | 2.04 | 2.99 | 3.63 |
| 19:00 | 5346 | Bremer SV vs BSV Rehden | 2.91 | 3.45 | 2.15 |
| 19:00 | 5802 | Musa Pori vs Ilves 2 | 1.82 | 3.92 | 3.38 |
| 19:10 | 3754 | AL Hazm vs Jeddah Club | 1.91 | 3.04 | 4.02 |
| 19:30 | 1547 | Al-Shamal vs Al Arabi Doha SC | 3.79 | 3.74 | 1.76 |
| 19:30 | 2371 | RW Rankweil vs FC Lauterach | 2.46 | 3.64 | 2.39 |
| 19:30 | 2562 | CSD Barnechea vs Magallanes | 3.15 | 3.10 | 2.17 |
| 19:30 | 3451 | Desamparados vs Atletico Camioneros | 2.60 | 2.50 | 3.18 |
| 20:30 | 2080 | Bloemfontein Celtic vs Maritzburg Utd | 2.39 | 2.90 | 3.15 |
| 20:30 | 2182 | Bavois vs Juventus Zurich | 1.62 | 3.94 | 4.33 |
| 20:30 | 2213 | SV Todesfelde vs SV Gw Siebenbaumen | 1.35 | 5.31 | 5.90 |
| 20:30 | 3704 | FC Bulle vs Rapperswil | 2.13 | 3.58 | 2.85 |
| 20:30 | 3995 | Amazulu vs Golden Arrows | 2.12 | 2.86 | 3.87 |
| 20:30 | 4251 | Chippa Utd vs TS Galaxy FC | 2.30 | 2.81 | 3.46 |
| 20:30 | 4648 | Orlando Pirates vs Marumo Gallants FC | 1.59 | 3.50 | 6.01 |
| 20:30 | 4673 | Juventud Unida G vs Douglas Haig | 3.52 | 2.69 | 2.25 |
| 21:00 | 1150 | Uruguay Montevideo FC vs CA Progreso | 2.75 | 2.90 | 2.55 |
| 21:00 | 1928 | Etoile Carouge FC vs SC Bruhl | 1.96 | 4.20 | 3.00 |
| 21:00 | 4228 | CD Villa Espanola vs IA Sud America | 2.26 | 2.90 | 3.20 |
| 21:30 | 1368 | Juventud LP vs CA Cerro | 2.60 | 2.85 | 2.75 |
| 21:30 | 5061 | Sansinena vs Sol de Mayo | 2.31 | 2.70 | 3.38 |
| 21:45 | 1576 | Wycombe vs Bristol City | 2.87 | 3.42 | 2.30 |
| 21:45 | 1671 | Brechin City vs Stirling | 3.83 | 4.12 | 1.68 |
| 21:45 | 3620 | Forest Green vs Brighton | 6.85 | 4.54 | 1.41 |
| 21:45 | 4086 | Leeds vs Barnsley | 1.26 | 5.45 | 10.09 |
| 21:45 | 4596 | Tranmere vs Newcastle | 11.01 | 5.60 | 1.24 |
| 21:45 | 4901 | Celtic Glasgow B vs Livingston FC B | 1.13 | 7.28 | 12.78 |
| 21:45 | 5485 | Edinburgh City vs Stranraer | 2.21 | 3.53 | 2.74 |
| 22:00 | 1284 | Trabzonspor vs Copenhagen | 2.00 | 3.50 | 3.40 |
| 22:00 | 1643 | Buckie Thistle FC vs Brora Rangers | 1.97 | 4.04 | 2.90 |
| 22:00 | 2853 | Dinamo Zagreb vs Bodo Glimt | 1.80 | 3.81 | 3.81 |
| 22:00 | 5641 | PSV Eindhoven vs Rangers | 1.75 | 3.85 | 4.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatano Agosti 24, 2022

Nipashe



Ten Hag afurahia kuitungua Liver

UKURASA 21

ACHENI WAJE...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), wakiwa mazoezini katika viwanja vya JK Park jijini Dar es Salaam kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Uganda itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Manzoki rasmi Dar

## Simba yafunguka dili lake na Vipers, safari ya kukiwasha Sudan...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiendelea kufanya mazungumzo na viongozi wa Vipers ya Uganda, kuhusu kukamilisha mpango wa kumsajili rasmi mshambuliaji Cesar Manzoki, mwenye uraia wa DR Congo na Afrika ya Kati, nyota huyo mkali wa kucheka na nyavu, ametua kimyakimya jijini Dar es Salaam kukamilisha 'dili' hilo, imefahamika.

**Nyota huyo aliingia nchini juzi usiku ikidaiwa kwamba ujio wake ni baada ya Simba kukubali kutoa ada inayokadiriwa kuwa Sh. milioni 233 ambazo Vipers imelazimika kukubali kiasi hicho badala ya Sh. milioni 400 ilizokuwa ikitaka awali, hiyo ikitokana na Manzoki kugoma kuichezea.**

Taarifa zilizolifikia gazeti hili muda mfupi kabla ya kwenda mitamboni jana kutoka kwa chanzo chetu cha uhakika, zilieleza kwamba nyota huyo yuko nchini tangu juzi usiku na amejichimbia katika moja ya hoteli jijini Dar es Salaam na huenda akawa sehemu ya kikosi kitakachoelekea Sudan kesho kwa mechi za kirafiki kama mambo yatakwenda sawa kati ya Simba na waajiri wake wa zamani, Vipers.

"Kuhusu suala la Manzoki, mashabiki wakae kwa kutulia kwa sababu (muda utaongea) ni mchezaji wa Simba na yupo hapa toka juzi ana mambo yake anafanya," alisema mtoa habari huyo.

Kuhusu nani atatemwa kumpisha kinara huyo wa ufungaji wa Ligi Kuu Uganda msimu uliopita, mtoa habari wetu alisema suala hilo liko chini ya Kocha Mkuu, Mserbia Zoran Maki.

"Kwa sasa hatutaki kuingilia mapendekezo ya benchi la ufundi, anaposema tunahitaji mchezaji fulani, basi tunatekeleza mahitaji yake kulingana anachokihitaji kikosini kuelekea michuano iliyopo mbele yetu, nani atampisha Manzoki hilo ni juu ya kocha mwenyewe," alisema.

Kwa mujibu wa Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema suala la Manzoki bado wanalifuatilia na wako katika mipango mizuri ya kufanikisha kupata saini ya nyota huyo.

Alisema bado hawajamalizana na Vipers, lakini mazungumzo yanaendelea kuhakikisha wanafanikiwa kumpata mchezaji huyo kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji.

"Manzoki ni mchezaji halali wa Vipers na bado ana mkataba, Simba tumejaribu kumfanya mazungumzo na klabu yake, lakini mambo hayajawa vizuri, ila bado tunaendelea na harakati za kumpata nyota huyo," alisema Ahmed.

Kikosi cha Simba kikiwa bila wachezaji wanane walioitwa kuitumikia Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), kesho kitakwea pipa kuelekea Sudan kushiriki michuano maalum ya kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika iliyoandaliwa na Mabingwa wa nchi hiyo, Al Hilal.

Katika michuano hiyo, Simba itacheza mechi mbili ambapo Jumapili wiki hii itaanza kwa kuivaa Asante Kotoko ya Ghana kabla ya Agosti 31, mwaka huu kuvaana na wenyeji, Al Hilal.

Baada ya mechi hizo, Simba itarejea Dar es Salaam na kucheza mechi moja kimataifa ya kirafiki dhidi ya AS Arta Solar 7 ya Djibouti, ambayo nayo imeweka kambi hapa nchini kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Yanga kujipima na kina Alex Song, Kalou

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha kikosi chao kinakuwa imara kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajia kuanza rasmi kati ya Septemba 9-11, mwaka huu, kikosi cha Yanga kitacheza mechi mbili za kirafiki kabla ya michuano hiyo kuanza, imeelezwa.

Moja kati ya timu ambayo Yanga itacheza nayo wakati huu Ligi Kuu Bara ikiwa imesimama kupisha Kalenda ya Fifa, itakuwa dhidi ya AS Arta Solar 7 ya Djibouti, ambayo kikosi chake kinaundwa na baadhi ya nyota wakubwa waliocheza klabu kubwa za Ulaya, wakiwamo Kiungo Mcameroon Alexander Song na winga Solomon Kalou raia wa Ivory Coast.

AS Arta Solar 7, ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Djibouti, wameweka kambi jijini Dar es Salaam kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika na katika hatua ya awali ya michuano hiyo itaanzia nyumbani dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan.

Kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, watakuwa na programu ya mazoezi na mechi za kirafiki kwa kipindi ambacho ligi imesimama kupisha Taifa Stars kucheza mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Uganda.

"Tunarudi katika mazoezi ya gym ili kujiweka sawa kwa kuwa tunaelekea katika michezo migumu, tulipumzika siku mbili kesho (leo) tunarudi kazini," alisema Kaze.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042